Nipashe
Jumamosi Novemba 21, 2020 Tanzania 1,000/- Kenya 100/-
ISSN 0856 • Na. 0580406
www.ippmedia.com
MWANGA WA JAMII
www.twitter.com/nipashetz www.facebook.com/nipashetz www.instagram.com/theguardian_newspaper
LIKE & FOLLOW US



**Balozi** akanusha Ulaya kuiwekea vikwazo Tanzania

UKURASA 3



**'Rais** wa Tanga' jela miaka 30 kwa kusafirisha dawa za kulevya

UKURASA 3

**Baba asisitiza Haaland haondoki Dortmund**

UKURASA 20

# KUMEKUCHA

• **CCM** yateua wagombea umeya, uenyekiti halmashauri, Kilolo, Mufindi zawekwa kiporo... *Endelea ukurasa 2*



Katibu wa NEC, Itikadi na Uenezi wa Chama Cha Mapinduzi (CCM), Hamphrey Polepole, akizungumza na waandishi wa habari, jijini Dar es Salaam jana, wakati akitangaza majina ya walioteuliwa na chama hicho kugombea nafasi za umeya wa majiji na manispaa, uenyeviti wa halmashauri za miji na wilaya. **PICHA: JUMANNE JUMA**

## YALIYOMO

UKURASA WA 4

### NEC YATAJA VIGINGI VINNE UCHAGUZI MKUU

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imetaja kero nne ilizokutana nazo wakati wa mchakato wa uchaguzi...

UKURASA WA 4

### MAJALIWA ATOA SIKU 15 HOSPITALI KUKAMILIKA

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa ametoa siku 15 kwa uongozi ya Wilaya ya Chamwino, Wakala wa Majengo...

## Kasi ya VVU kwa vijana yatisha

UKURASA 3



Scan Hapa
Fungua App ya QR Code Reader kisha scan kupakua APP yetu
Google Play App Store

# DPP aagiza TAKUKURU, DCI kuchunguza sakata la saruji

UK. 2

MICHEZO SIMBA SC, AZAM VITANI LIGI KUU UK.24 MAONI, KATUNI UK.6

HABARI KITAIFA

# Jaji Warioba awataka wanahabari kubadilika

**Na Romana Mallya**

WAZIRI Mkuu Mstaafu, Jaji Joseph Warioba, ameitaka Bodi mpya ya Baraza la Habari Tanzania (MCT) kusimamia vyombo vya habari kuandika habari za wananchi zaidi.

Bodi hiyo ambayo ilizinduliwa jana jijini Dar es Salaam, itaongozwa na Rais mpya wa Baraza hilo, Jaji Juxton Mlay na Makamu wake Yusuph Khamis Yusuph ambaye ni Mhariri wa Zanzibar Leo.

Wengine na nafasi zao kwenye mabano ni Tido Mhando (Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili), Eda Sanga (Makamu Mwenyekiti wa Kamati ya Maadili), Happiess Nkya (Mwenyekiti wa Bodi atakayesimamia Kamati ya Hesabu, Ukaguzi) na wajumbe ni Anna Henga, Dk. Joyce Bazira na Teddy Mapunda.

Alizungumzia katika uzinduzi huo, Jaji Warioba alisema vyombo vya habari vinatakiwa kujielekeza kwenye uandishi wa habari za wananchi badala ya kuegemea kuandika habari za viongozi pekee.

"Lazima mhakikishe vyombo vya habari vikomae zaidi. Wakati tunaingia ndiyo kipindi nchi imeingia kwenye mfumo wa siasa wa vyama vingi na habari zilikuwa nyingi na tumeendelea hivyo hivyo.

"Ila sasa sina uhakika, kama vyombo vya habari vimekomaa kiasi cha kutoa habari za kila aina kwa wananchi," alisema.

Jaji Warioba alisema wakati nchi ikiwa kwenye mfumo wa chama kimoja, vyombo vya habari vilikuwa vya serikali na vilitoa nafasi ya kutoa habari za wananchi.

"Vyombo vya habari vya sasa havitoi habari za kutosha za wananchi zaidi. Tunapata habari za uongozi na mara nyingi inakuwa kawaida kusema wananchi wapewe elimu. Tumesahau kwamba uongozi lazima upate elimu kutoka kwa wananchi, hivyo ni lazima maoni ya wananchi yaonekane kwenye vyombo vya habari," alisema.

Alipokuwa Waziri Mkuu na Makamu wa Kwanza wa Rais, alisema kupitia msaidizi wake alikuwa akimwandalia rundo la magazeti ambayo ameweka alama kwenye baadhi ya taarifa zilizomo na nyingi ambazo alipenda kuzisoma ni zile za barua za wasomaji za wananchi.

Rais wa MCT, Jaji Mlay, aliahidi baraza hilo litafanyia kazi suala hilo na kama mazingira yataonekana kuwa magumu watatoa mrejesho kwa wahusika pamoja na serikali ili kujenga mazingira hayo kwa kuwezesha wananchi kutoa sauti zao kwa yale wanayotaka kwa viongozi.

"Tutahakikisha yale wanayofikiria wananchi kuwa ni muhimu kwao kwenda kwa viongozi yanawafikia na yale ya kuchukua kwa viongozi kama mrejesho kwa wananchi nayo yanawafikia," alisema.

Naye, Katibu Mtendaji MCT, Kajubi Mukajanga, alisema hiyo ni bodi ya tisa tangu kuanzishwa kwake mwaka 1995 ambapo hufanya kazi yake kwa kipindi cha miaka mitatu.



Waziri Mkuu mstaafu, Jaji Joseph Warioba (wa pili kulia), akimkabidhi vitendea kazi Rais mpya wa Baraza la Habari Tanzania (MCT), Jaji mstaafu Juxon Mlay, baada ya kuzindua Bodi mpya ya baraza hilo, jijini Dar es Salaam jana. Kushoto ni Makamu wa Rais wa baraza hilo aliyemaliza muda wake, Hassan Mitawi na Katibu Mtendaji wa baraza hilo, Kajubi Mukajanga. **PICHA: JUMANNE JUMA**

# CCM yateua wagombea umeya, uenyekiti

**Na Romana Mallya**

CHAMA Cha Mapinduzi (CCM), kimepitisha wanachama wake kugombea nafasi za umeya wa majiji, manispaa, uenyekiti wa halmashauri miji na wilaya.

Wakati wanachama hao wakiteuliwa kugombea nafasi hizo, halmashauri wilaya za Kilolo, Mufindi, Mtwara, Njombe Nkasi na Msalala zimeagizwa kurudia upya mchakato wa kupata wagombea.

Akizungumza jana na waandishi wa habari, Katibu wa Halmashauri Kuu ya Taifa (NEC), Itikadi na Uenezi ya CCM, Humphrey Polepole, alizitaka kamati za madiwani kuanzia Jumatatu kufanya uchaguzi ndani ya siku mbili.

Polepole alisema Kamati Kuu ya Halmashauri Kuu ya Taifa iliyokutana mjini Dodoma chini ya Mwenyekiti Rais John Magufuli ilithibitisha wanachama hao kugombea nafasi hizo.

Alisema katika kuwapitisha wagombea hao, wamezingatia uadilifu, utendaji wa kazi, rushwa na ubadhirifu wa mali za umma.

Pia alisema Kamati Kuu ilitaka kujiridhisha watu kwamba pamoja na kwamba si malaika, wamevuka kiwango cha kawaida kwa kuwa waaminifu, wachapa kazi, waadilifu, wanyenyekevu, wanaweka mbele maslahi ya umma na kufuata maelekezo ya serikali.

Alisema kati ya waliothibitishwa kuna maeneo ambayo jina limerudi moja na kwingine mawili hadi matatu na baadhi wametakiwa kurudia mchakato huo na watakaopatikana kwenye halmashauri ndiyo watakaogombea nafasi hizo na vyama vingine.

Akitaja majina ya nafasi ya umeya katika majiji na idadi ya waliojitokeza kwenye mabado, Polepole alisema Dar es Salaam (9), Arusha (17), Dodoma (7), Tanga (6), Mwanza (7), Mbeya (10).

Katika nafasi ya mameya wa manispaa, alisema zipo 20 lakini waliojitokeza walikuwa 150, nafasi za wenyeviti wa halmashauri za wilaya 137 waliojitokeza ni 682 na nafasi za wenyeviti wa halmashauri za miji 22 waliojitokeza ni 109.

Aidha katika Jiji la Dodoma, aliyekuwa Meya katika kipindi kilichopita, Prof. David Mwamfupe, amerejeshwa peke yake kugombea nafasi hiyo.

MAJINA ZAIDI YA MOJA

Polepole aliwataja waliothibitishwa kugombea nafasi za umeya Halmashauri ya majiji kuwa ni Arusha (Maxmillian Irankre, Prosper Msofe na Isaya Doita), Dar es Salaam (Mariam Luida, Adinani Kondo na Omari Matulanga), Mbeya (Daudi Ngogo, Duru Rahmati na Daniel Mwaibidi), Mwanza (Biku Kotecha, Edith Mudogo, Nasima Sima) na Tanga (Abdulrahiman Shiloo, Saidi Rashidi na Ahmed Mwinjaga).

**MMOJA MMOJA MANISPAA**

Polepole alizitaja manispaa ambazo wagombea limerudi jina moja moja Ilala (Omar Kumbilamoto), Kigamboni (Ernest Ndago), Moshi (Juma Rahibu), Shinyanga (David Mkulila), Bukoba (Godson Jigson), Mpanda (Haidari Hemedi) na Ilemela (Renatus Mulunga).

**ZAIDI YA MMOJA**

Katika manispaa ambazo wamethibitishwa zaidi ya mmoja ni Ubungo (Ester Ndoha na Jafari Nyaigesha), Kinondoni (Leonard Manyama, Manfred Lioto na Songoro Mnyonge), Temeke (Juma Mkenga na Abdallah Mtimika).

Lindi (Frank Rafael, Juma Mpendakulya na Seleman Laus), Songea (Michale Mbano, Issa Mkwawa na Osmund Kapinga), Tabora (Alfonce Kurwa, Mhamad Yahya na Ramadhan Kapera) na Mtwara (Haruni Selemani, Lamek Sylvester na Shadida Ndile).

Zingine ni Sumbawanga (Justine Malisawa, Frank Bulongo na Charles Chapewa), Iringa (Jackson Chaula, Ibrahimu Mwangwada na Thadeus Tenga), Kigoma Ujiji (Baraka Lupori, Sharon Mashanya na Musa Ibrahim), Singida (Yadi Kialatu, Gwaijima Mbua na Kipandwa Ipini).

Manispaa ya Musoma ni (Jumbura Lugora na William Gumbo) na Morogoro ni (Paschal Kihanga, Seif Changoka na Mhandisi Hamis Ndwata).

# DPP aagiza uchunguzi sakata ya saruji

**Na Beatrice Moses**

MKURUGENZI wa Mashtaka (DPP), Biswalo Mganga, ameagiza Mkurugenzi wa Upelelezi na Makosa ya Jinai (DCI) na Taasisi ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU), kuchunguza kama kuna hujuma zinazofanywa na baadhi ya wafanyabiashara kwenye uuzaji wa saruji.

Katika taarifa yake, DPP Mganga aliziagiza taasisi hizo kuanza uchunguzi wa hujuma hizo jana na kutakiwa kukamilisha ndani ya siku 30.

DPP Mganga alisema: "Katika kipindi cha takribani mwezi mmoja nimebaini uwapo wa tatizo la kupanda kwa bei ya saruji na vifaa vya ujenzi katika mikoa mbalimbali nchini."

Alisema mazingira ya suala hilo yanaashiria uwapo wa makosa ya jinai katika mnyororo wa uzalishaji na uuzaji wa bidhaa hiyo kwa wateja, hivyo kusababisha kuuzwa na kununuliwa kwa bei ya juu au kutopatikana sokoni.

"Ikumbukwe kuwa ni kosa la uhujumu uchumi kwa mujibu wa Sheria ya Uhujumu Uchumi na Uhalifu wa Kupangwa sura 200 Marejeo 2019, inayoelezwa kuwa kwa mtu yeyote mwenye leseni au asiye na leseni kufanya biashara kukutwa na bidhaa katika mazingira yanayoashiria kuunyima umma fursa ya kuinunua bidhaa husika kwa bei stahiki, kuuza bidhaa kwa bei au kwa masharti yaliyo na sheria," alisema Mganga.

Alisema sheria hiyo inabainisha kuwa wakati wa kufanya biashara husika, kutengeneza katika makusudi mazingira yanayoweza kusababisha uhaba wa bidhaa katika soko.

Pia alisema kuwapo kwa ongezeko kubwa au kupungua kwa bei katika soko kinyume cha sheria kuna athari katika mgawanyo sawa na usambazaji wa bidhaa katika soko na kwa wanunuzi katika eneo husika.

Mkurugenzi huyo alibainisha kuwa atakapopokea jalada husika la uchunguzi, atachukua hatua za kisheria kwa kuzingatia misingi inayomuongoza kama ilivyoainishwa katika ibara ya 59 ya Katiba ya Jamhuri ya Muungano wa Tanzania ya mwaka 1977 na sheria zingine za nchi.

Kuadimika kwa saruji na kupanda bei katika baadhi ya maeneo nchini, kulisababisha usumbufu kwa wananchi na taasisi zinazohitaji bidhaa hizo, kwa ajili ya ujenzi wa majengo na miundombinu tofauti.

Nipashe, mwanzoni mwa mwezi huu, iliibua kupanda kwa bei ya saruji katika maeneo mbalimbali nchini, hali iliyowasukuma mamlaka husika wakiwamo wakuu wa mikoa kuanza kufanya operesheni katika maduka.

Kadhalika, Waziri Mkuu Kassim Majaliwa wakati akiapishwa mjini Dodoma, alitoa tamko la kuanza kuwashughulikia wafanyabiashara wote waliohujumu bidhaa hiyo.

HABARI KITAIFA

# Maambukizi VVU kwa vijana yatisha

**Na Edwin Mhagama**

HALI ya UKIMWI nchini bado ni tishio na serikali imesema kwamba wastani wa watu wanane wanaambukizwa virusi vya UKIMWI (VVU) ambao ni sawa na watu 72 kwa siku.

Kwa mujibu wa serikali, hali hiyo inatokana na ongezeko kubwa la maambukizi ya VVU kwa vijana wenye umri kuanzia miaka 15 mpaka 35 na kwamba hatua hiyo, inachangia maambukizi mapya kwa zaidi ya asilimia 50.

Katibu Mkuu Ofisi ya Waziri Mkuu, Sera, Uratibu na Uwekezaji, Dorothy Mwaluko, alipokuwa akitangaza wiki ya kuelekea kilele cha kuadhimisha Siku ya UKIMWI Duniani itakayofanyika Desemba Mosi. Maadhimisho hayo kitaifa kwa mwaka huu yatafanyika Moshi, mkoani Kilimanjaro.

"Kwa nchi yetu, hali ya maambukizi mapya ya UKIMWI bado ni tishio. Takwimu zinaonesha kuwa takribani watu 72,000, hupata maambukizi mapya ya ukimwi kwa mwaka, sawa na wastani wa watu 6,000 kwa mwezi na watu 200 kwa siku au watu wanane kwa kila saa moja" alisema Mwaluko.

Alisema kutokana na takwimu za UKIMWI kutoridhisha na kuhatarisha mustakabali wa taifa, ni jukumu la kila mwananchi, hususani vijana, kuhakikisha mipango na mikakati iliyowekwa na serikali ya kupambana na UKIMWI inatekelezwa ili kuzuia maambukizi mapya.

"Mikakati hiyo tunatekeleza katika makundi mawili. Wale ambao wamekwishaambukizwa ili kuwawezesha kufubaza virusi na kundi la pili ni wale ambao bado hawajaambukizwa. Lazima kuwapo na jitihada za kuhakikisha hawapati maambukizi" aliongeza.

Awali, Mwaluko alisema katika maadhimisho ya mwaka huu ambayo yatafanyika katika mji wa Moshi mkoani Kilimanjaro, mgeni rasmi anatarajiwa kuwa Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, na kuwataka vijana kushiriki kikamilifu katika shughuli hiyo.

Maadhimisho ya mwaka huu yanaongozwa na kaulimbiu inayosema 'Mshikamano wa Kimataifa Tuwajibike kwa Pamoja'.

Maadhimisho ya Siku ya UKIMWI Duniani hufanyika Desemba Mosi kila mwaka na yaliasisiwa na Shirika la Umoja wa Mataifa linaloshughulikia UKIMWI (UNAIDS) mwaka 1988 kwa lengo la kutathmini hali halisi na mwelekeo wa kudhibiti maambukizi ya ugonjwa huo.

## Balozi akanusha vikwazo Tanzania

**Na Beatrice Moses**

BALOZI wa Tanzania nchini Ubelgiji na Mwakilishi katika Umoja wa Ulaya, Jestas Nyamanga, amekanusha taarifa kuwa Bunge la Ulaya limeiwekea vikwazo vya kiuchumi Tanzania na kuifungia mikopo na misaada.

Kutokana na ufafanuzi huo, Balozi Nyamanga amewataka Watanzania kupuuza taarifa hizo, alizoziita kuwa ni za upotoshaji.

Taarifa zilizotolewa hivi karibuni zilisema Tanzania kutokana na vikwazo hivyo, itakosa Sh. tilioni 1.6.

Katika video iliyorushwa kwenye mitandao kadhaa ya kijamii na kuonyeshwa mara kwa mara kwenye kituo cha Luninga ya Shirika la Utangazaji Tanzania (TBC), Balozi Nyamanga anabainisha kuwa hakukuwa na kikao cha bunge bali kamati ya mambo ya nje ya bunge hilo.

" Leo (juzi) tarehe 19 asubuhi hapa Ubelgiji, Kamati ya Bunge ya Mambo ya Nje ya Umoja wa Ulaya, ilikutana katika kikao chake cha kawaida. Miongoni mwa masuala yaliyojadiliwa katika kamati hiyo ilihusu Tanzania na hali ilivyo baada ya uchaguzi mkuu kukamilika.

"Huu ni utaratibu wa kawaida kabisa kujadili na kuweka majadiliano kuhusu mbia wao mkuwa wa maendeleo pindi tu uchaguzi unapokuwa umekamilika na hasa uchaguzi mkuu, " alisema. Balozi Nyamanga alisema taarifa ya kuwa Bunge la Ulaya limeazimia kuiwekea Tanzania vikwazo ni upotoshaji unaozushwa na watu wasioitakia nchi mema.

"Taarifa hizi ni za uongo hazina ukweli wowote. Kikao hicho cha kamati ya bunge hakikutoa azimio lolote kuhusu Tanzania. Kilichofanyika ni kuwapa wabunge kutoa mawazo yao kuhusu hali ya Tanzania baada ya uchaguzi," alisisitiza.

Alibainisha kuwa kikao ni cha Kamati ya Mambo ya Nje ya Bunge la Umoja wa Ulaya yenye wabunge 71 na si bunge zima na kwamba wabunge katika vikao vyao kila mmoja ana haki ya kutoa mawazo yake.

Balozi Nyamanga alisema Bunge la Ulaya lina wabunge 705 na kama ilivyo Tanzania, wabunge wana haki ya kutoa mawazo yao, hivyo katika kikao hicho, wabunge hao watao walitoa mawazo tofauti tofauti wanavyoona lakini hakuna azimio lililotolewa.

"Si kweli kuwa fedha hizo zimesitishwa, utekelezaji wa miradi mbalimbali unaendelea tena vizuri na hakuna zuio lolote la kusitisha fedha hizo," alisema.

Alisema pia hakuna mjadala wowote unaoendelea kwenye Bunge la Ulaya kuhusu kuiwekea Tanzania vikwazo ikiwamo kuuza bidhaa zake katika nchi hizo.




Mkurugenzi Msaidizi wa Ofisi ya Mashtaka nchini, Faraji Nchimbi, akizungumza na waandishi wa habari jijini Tanga jana, baada ya Mahakama ya Uhujumu Uchumi Tanga, kumhukumu mfanyabiashara wa mkoani humo, Yanga Omary maarufu kama Rais wa Tanga, kwenda jela miaka 30 kwa kujihusisha na biashara ya dawa za kulevya. **PICHA: BONIFACE GIDEON**

## 'Rais wa Tanga' jela miaka 30 kusafirisha dawa za kulevya

**Na Boniface Gideon** ,TANGA

JANA Mahakama Kuu, Kanda ya Tanga, Divisheni ya Uhujumu Uchumi na Rushwa maarufu Kama Mahakama ya Mafisadi, imemhukumu mfanyabiashara Yanga Omary maarufu kama 'Rais wa Tanga', kifungo cha miaka 30 baada ya kumkuta na hatia ya kusafirisha gramu 1052.63 ya dawa za kulevya aina ya Heroine.

Hukumu hiyo iliyohudhuriwa na wakazi wengi wa Mkoa wa Tanga imetolewa na Jaji Immakulata Banzi leo jijini hapa .

Akitoa hukumu hiyo, Jaji Immakulata Banzi alisema ametoa adhabu hiyo baada kusikiliza maelezo ya pande zote na kumkuta na hatia ya kujihusisha na dawa za kulevya.

Pamoja na hukumu hiyo Jaji banzi alisema mali za Omary likiwamo gari aina ya Toyota Landcruiser, ambalo alikutwa nalo akiwa amehifadhi dawa, hazitataifishwa kwa kuwa sio mali zake.

Hata hivyo, mahakama hiyo iliwaachia huru mke wa mfanyabiashara huyo, Rehema Ally, na mfanyakazi wa ndani, Halima Mohamed, baada ya kukosekana ushahidi kuwa walijihusisha na biashara hiyo.

Ilidaiwa mahakamani hapo kuwa Agosti na Oktoba, 2018 mshtakiwa huyo na wenzake wawili walikamatwa mtaa wa Bombo jijini Tanga wakitaka kusafirisha dawa hizo za kulevya.

Akizungumza nje ya Mahakama, Mkurugenzi Msaidizi wa Mashtaka, Faraja Nchimbi, alisema hukumu ni mwendelezo wa kesi za watu wanaojihusisha na biashara haramu ya dawa za kulevya nchini .

Aliwataka watu wanaojihusisha na biashara hiyo kuacha mara moja kwa kuwa serikali itawashughulikia wote pamoja na kuvunja mitandao ya watu hao.


## KUMBUKUMBU



ROSE SIMON IVAMBI
2009 - 2020

**NI MIAKA KUMI NA MOJA (11)** SASA YA MAJONZI NA UPWEKE WA KUONDOKEWA NA MPENDWA MAMA YETU. ULITUSHIKA MIKONO WAKATI TUKIWA WADOGO, WEWE NDIYE SHUJAA WA UTOTO WETU NA MIAKA YA BAADAYE PIA. KILA TUKIKUFIKIRIA MIOYO YETU HUJAZWA NA FURAHA. TUNAKUKUMBUKA KILA WAKATI KWA KICHEKO NA HUZUNI. TUNAMSHUKURU MUNGU KWA KUTUPATIA **ZAWADI YA MAMA** WA AINA YAKO. ***DAIMA UPO MIOYONI MWETU.***

**UNAKUMBUKWA DAIMA NA WANAO: *VERONICA, SEBASTIAN, OLIVA, JANETH NA FRIDA, WAJUKUU ZAKO:HANS, LOUIS, MARTIN, AGATHA, SIMON SENIOR, BENARD, MARICELLA, SIMON JUNIOR, STEVIE, NANCY JUNIOR, NANCY SENIOR NA DIANA, WAKWE ZAKO, NDUGU NA MAJIRANI***

**DAIMA TUNAKUOMBEA,**
**MAMA ROHO YAKO IPUMZIKE KWA AMANI.**

**BWANA ALITOA NA BWANA AMETWAA JINA LA BWANA LIHIMIDIWE**

# Majaliwa atoa siku 15 hospitali kukamilika

**Na Mwandishi Wetu**

WAZIRI Mkuu Kassim Majaliwa ametoa siku 15 kwa uongozi ya Wilaya ya Chamwino, Wakala wa Majengo Tanzania (TBA) na Shirika la Uzalishaji Mali la Suma JKT, kuhakikisha ujenzi wa hospitali ya Uhuru katika Halmashauri ya Chamwino, unakamilika.

Akizungumza baada ya kukagua maendeleo ya ujenzi wa hospitali hiyo, Waziri Mkuu alisema lengo ni kuhakikisha hospitali hiyo inazinduliwa na Rais John Magufuli, ifikapo Desemba 9, mwaka huu.

"Nimeridhika na hatua hii ya ujenzi lakini haitoshi, hamieni hapa, huu ni wakati wa kazi, hakikisheni kazi inafanyika usiku na mchana ili Desemba 5, 2020 kazi ikamilike na Desemba 9, 2020 izinduliwe," alisema Majaliwa.

Aidha, Waziri Mkuu alisema kuwa anataka kuona vifaa vyote vya ujenzi wa hospitali hiyo vinatoka kwenye viwanda vya ndani, ili kuharakisha ukamilishwaji wa hospitali hiyo hasa marumaru, kwani kuna viwanda vikubwa nchini vinavyozalisha bidhaa hiyo kwa ubora.

"Mnabishana kuhusu uwekaji wa marumaru, mnataka za nje? TBA mnang'ang'ania kununua marumaru kutoka nje ya nchi, kwa nini? Sisi tumehamasisha ujenzi wa viwanda na viwanda vipo vinavyotengeneza marumaru tena nzuri," alisema Majaliwa na kuongeza:

"Tuna kiwanda Chalinze kikubwa sana na kingine kipo Mkuranga, hata jengo letu la Tume ya Taifa ya Uchaguzi tumeweka marumaru za ndani, na bora mshitiri hujazinunua, na usinunue kutoka nje, tuna viwanda vipo nchini," amesisitiza Majaliwa.

Akitoa taarifa ya ujenzi wa hospitali hiyo, Katibu Mkuu Ofisi ya Rais (TAMSEMI), Mhandisi Joseph Nyamhaga, alisema ujenzi wa hospitali hiyo ni utekelezaji wa agizo la Rais Magufuli alilolitoa kuwa Sh. milioni 995.1 zilizokuwa zimetengwa kwa ajili ya maadhimisho ya miaka 57 ya uhuru mwaka 2018, zitumike katika ujenzi wa hospitali hiyo.

Pia, Januari 2019, wakati akipokea gawio la hisa za kampuni ya simu ya Airtel, aliagiza kiasi cha Sh. bilioni 2.415 zitumike kwenye ujenzi huo.

Alisema hadi kufikia Novemba 19, mwaka huu, Sh. Bilioni 4,430 zilipokelewa kwa ajili ya ujenzi wa hospitali hiyo, kwamba kati ya kiasi hicho Sh. milioni 368.411 hakijatumika.

Alisema kwa mwaka 2020/2021, serikali imepanga kuendelea na ujenzi wa hospitali za halmashauri 27 ambazo kila moja imetengewa Sh. bilioni moja.

Aidha, alisema Sh. bilioni 27.75 zimetengwa kwa ajili ya ujenzi



Waziri Mkuu Kassim Majaliwa, akikagua ujenzi wa Hospitali ya Uhuru, wilayani Chamwino, mkoani Dodoma jana. Kushoto ni Mkuu wa Mkoa wa Dodoma, Dk. Bilinith Mahenge. **PICHA: OWM**

# NEC yataja vigingi vinne uchaguzi mkuu

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

TUME ya Taifa ya Uchaguzi (NEC), imetaja kero nne ilizokutana nazo wakati wa mchakato wa uchaguzi mkuu uliofanyika Oktoba 28, mwaka huu, ikiwamo baadhi ya wagombea kuwatisha wasimamizi.

Mkurugenzi wa Uchaguzi wa NEC, Dk. Wilson Charles, aliyasema hayo jana wakati wa kikao cha tathmini ya uchaguzi mkuu wa mwaka 2020 kilichohudhuriwa na waratibu wa uchaguzi wa mikoa na wasimamizi wa majimbo yote nchini.

Alisema licha ya mafanikio yaliyopatikana kulikuwa na kero chache, kwamba katika uchaguzi huo kulikuwa na vitisho vya simu kwa wasimamizi kuanzia ngazi ya majimbo hadi taifa.

"Tunashukuru Mungu jambo limeisha maana kulikuwa na vitisho na matusi ambavyo vilikuwa vikitolewa na baadhi ya viongozi wa vyama kwa wasimamizi na Mkurugenzi wa Uchaguzi kwa njia ya simu," alisema Dk.Charles.

Alitaja kero nyingine kuwa ni kutozingatiwa kwa ratiba za kampeni za uchaguzi na kuingilia ratiba za wagombea wengine.

"Kulikuwa na mwingiliano wa ratiba, baadhi ya vyama vilikuwa vikiingilia ratiba za vyama vingine katika mikutano ya kampeni za uchaguzi na kugoma kushuka jukwaani,"alisema Dk.Charles.

Alisema kulikuwapo na wagombea ambao walikuwa wanapitisha muda uliopangwa wa kunadi sera zao pindi walipokuwa jukwaani.

"Kulikuwa na tatizo la wagombea kupitisha muda wa saa 12 jioni uliopangwa wa kufanya kampeni, mtu anakataa waziwazi anaambiwa shuka anasema sishuki, lakini nawapongeza askari kwa kuchukua hatua sasa hayo yamepita,"alisema Dk. Charles.

Alitaja kero nyingine ni baadhi ya vyama vya siasa wagombea wake kutokutii maagizo ya Kamati ya Maadili.

"Baadhi ya vyama vya siasa kutotii wito wa Kamati ya Maadili na ukiukwaji wa maadili wakati wa mchakato mzima wa kampeni, hili nalo lilijitokeza,"alisema Dk. Charles.

Kadhalika, alitaja kero ya nne kuwa ni idadi kubwa ya rufaa walizozipokea ikilinganishwa na uchaguzi wa mwaka 2015. "Kulikuwa na pingamizi za kutosha sijui ni kwa sababu ipi? Lakini mengi yalikuwa ya wagombea kwa wagombea. Hii ilituletea shida kupitia na rufani zilikuwa nyingi," alisema Dk. Charles.

Aidha, alisema idadi ya wapigakura katika uchaguzi huo ilikuwa ni asilimia 51 ambapo idadi hiyo ni kubwa ikilinganishwa na uchaguzi wa mwaka 2015 iliyokuwa asilimia 49.

Aidha, alibainisha kuwa asilimia 17 ya wagombea wa nafasi za ubunge na udiwani ambao wameshindwa kurudishwa baada ya kukata rufaa ni kutokana na kukosa sifa na kama wataenda mahakamani hawatashinda.

Dk. Charles alisema asilimia 83 ya rufaa zilizokatwa waliwarejesha kwenye uchaguzi, huku asilimia 17 hawakurudishwa.

# Wavuvi kicheko kuanzishwa wizara ya uchumi wa buluu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

SIKU moja baada ya Rais wa Zanzibar, Dk. Hussein Mwinyi kuunda Baraza la Mawaziri, wadau wa uvuvi wamepongeza kuazishwa kwa wizara mpya ya uchumi wa bluu na uvuvi.

Wakizungumza jana na Nipashe kwa nyakati tofauti, wadau hao walipongeza hatua ya Rais Mwinyi ya kuunda wizara hiyo hali inayoonyesha kwamba serikali ya awamu ya nane imepania kuendeleza sekta ya uvuvi ili kuinua uchumi wa Zanzibar.

Mwenyekiti wa Jumuiya ya Maendeleo wa Wavuvi wa Kojani, Omar Muhammed Ali, alisema anampongeza Dk. Mwinyi kwa kuonyesha juhudi za kuboresha sekta ya uvuvi kutokana na ukweli kwamba kijiografia Zanzibar imezungukwa na bahari na wananchi wake wanategemea uvuvi.

Alisema wakazi wengi wa Zanzibar wanategemea bahari kama sehemu ya kimbilio salama, hivyo kuanzishwa na wizara hiyo ni jambo jema na wako tayari kutoa ushirikiano kwa serikali.

Hata hivyo, alishauri watendaji watakaopewa dhamana akiwamo waziri wa wizara hiyo, wajue wana wajibu wa kusimamia majukumu ya kuendeleza uvuvi na kuwa karibu sana na wavuvi.

Aliomba kuwekwe mazingira rafiki ambayo yatatekelezeka baina ya waliopewa dhamana ya kusimamia wizara hiyo na wavuvi wenyewe.

"Tunaomba kuwe na vikao vya mara kwa mara kubadilishana mawazo, kupitiwa kwa Sheria ya Uvuvi ya mwaka 2010 ambayo imetoa mamlaka ya kudhiti maeneo ya bahari," alisema.

Naye Ofisa Teknolojia ya habari na mawasiliano (TEHAMA) wa Mamlaka ya Kusimamia Uvuvi wa Bahari Kuu, Muhammed Khamis Mwamvura, alisema wizara hiyo mpya ina muono mkubwa na italeta manufaa kwa Zanzibar kwa sababu uchumi wa buluu si uvuvi pekee bali hata utalii, hivyo Zanzibar itakua kiuchumi.

Alisema kuwa hata Rais wa Tanzania, Dk John Magufuli, alisema atanunua meli nane za uvuvi wa bahari kuu ambazo kati ya hizo nne zitaletwa Zanzibar, hivyo uchumi wa buluu utaleta neema kubwa.

Muhammed alisema Rais Mwinyi katika kampeni zake alisema atajenga bahari ya uvuvi, hivyo pia viwanda vya kuchakata samaki vitajengwa na Wazanzibari watanufaika kupitia mazao ya baharini.

"Wizara hii ya uchumi wa buluu na uvuvi ni wizara mama kulingana na sera ya Rais wa Zanzibar, Dk. Mwinyi, ambayo ameipa kipaumbele," alisema.

Katibu wa Ushirika wa Wakulima Hai unaoshughulika na Majongoo Bahari Zanzibar, Semeni Mohammed, alisema ukulima wa majongoo una faida kubwa, hivyo kuanzishwa kwa wizara hiyo kutasaidia kutatua kwa matatizo katika ufugaji huo.

Alisema hakuna mazingira rafiki katika shughuli hiyo hasa katika usafirishaji wa majongoo bahari nje ya nchi ambako yana soko kubwa duniani hasa nchini China.

"Tunataka tutambulike kuwa ufugaji wa majongoo bahari na ni moja ya uchumi ambao utatoa ajira nyingi kwa watu wa ukanda wa pwani hasa ikizingatiwa soko lake ni kubwa na wateja wanatusubiri kupeleka bidhaa zetu," alisema.

Naye Mkurugenzi Mkuu wa Shirika la Uvuvi Zanzibar (ZAFICO), Zahor Kassim, alisema anapongeza kuanzishwa kwa wizara hiyo na kwamba shirika lake lina miradi mbalimbali ya kuendeleza uvuvi ikiwama kujenga kiwanda cha kuchakata dagaa na samaki.

IPP



# Salamu za Pongezi

## Mhe. Majaliwa Kassimu Majaliwa

Uongozi na wafanyakazi wa kampuni za **IPP** wanaungana na Watanzania wote kumpongeza Mheshimiwa Kassim Majaliwa kwa kuteuliwa na Mhe. Rais Dk. John Pombe Magufuli kuwa Waziri Mkuu wa Jamhuri ya Muungano wa Tanzania .

***Hongera sana.***

Nipashe
MWANGA WA JAMII

# Ligi Kuu Bara irejee na ubora, burudani

**TIMU** zinazoshiriki Ligi Kuu Bara zimerejea tena katika vita ya kuwania ubingwa wa ligi hiyo baada ya kumalizika kwa kalenda ya kimataifa ambapo kwa Tanzania (Taifa Stars), ilikuwa inakabiliwa na mchezo miwili ya ugenini na nyumbani dhidi ya Tunisia.

Mechi hizo mbili zilikuwa ni kwa ajili ya kusaka tiketi ya kushiriki fainali zijazo za Kombe la Mataifa ya Afrika (Afcon 2022), ambazo zitafanyika nchini Cameroon.

Ligi Kuu Tanzania Bara ambayo inashirikisha timu 18 kutoka mikoa mbaliambali, imerejea kuanzia jana kwa timu sita kushuka kwenye viwanja vitatu tofauti ili kusaka pointi tatu muhimu zitakazowapeleka kwenye malengo yao ya msimu huu.

Timu nyingine nane zitashuka dimbani leo wakiwamo mabingwa watetezi, Simba ambayo imewafuata Coastal Union jijini Arusha, wakati raundi ya 11 itakamilika kesho kwa Yanga kuwakaribisha Namungo FC kwenye Uwanja wa Uhuru, Dar es Salaam, huku Mwadui FC ikiwafuata Kagera Sugar kwenye Uwanja wa Kaitaba, Mjini Bukoba.

Ili ligi hiyo ya ngazi ya juu kwa upande wa Tanzania Bara ionekane kuwa bora na ya thamani ni vyema timu zote zikaingia uwanjani kuonyesha soka la kiwango cha juu.

Timu itakayoonyesha ubora katika mechi zake zote, itajiweka kwenye mazingira mazuri ya kupata ushindi au kuambulia sare dhidi ya mpinzani wake.

Mbali na kupata pointi, ambalo ndio lengo kuu kwa kila timu, lakini wachezaji husika hujiweka sokoni kwa kuzivutia klabu nyingine ambazo zinahitaji kujiimarisha kwa kusajili nyota wapya mara baada ya dirisha dogo la usajili litakapofunguliwa mwezi ujao.

Mpira wa miguu ni mchezo wa hadharani, hivyo kila ambaye ataitumia vyema nafasi ya kujituma, kucheza kwa kiwango cha juu na kudumisha nidhamu ndani na nje ya uwanja, atakuwa amejiweka jirani au amejifungulia njia ya mafanikio.

Nipashe inaamini wakati ligi imesimama kupisha timu za taifa mbalimbali kuendelea na majukumu yake, makocha wametumia nafasi ya kurekebisha makosa waliyoyaona kwenye mechi 10 zilizotangulia, na sasa wako tayari kuwapa mashabiki na wanachama wao burudani.

Ni wazi timu ambayo itarejea uwanjani ikiwa na mipango ya kucheza kandanda safi, itajipatia ushindi lakini pia itawaweka wachezaji wake 'sokoni' kutokana na burudani ambayo wataionyesha katika kila mchezo.

Tunaamini Kamati ya Waamuzi iliyoko chini ya Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), pamoja na Bodi ya Ligi Kuu imetumia pia muda huo wa mapumziko kuwajengea uwezo zaidi waamuzi wake kwa ajili ya kufanya vyema kazi yao.

Kufanya vizuri kwa waamuzi, ni sehemu mojawapo inayotegemewa katika kuwajenga wachezaji wetu na hatimaye kupata wawakilishi wa mashindano ya kimataifa ambao wameiva na hawakupatikana kwa njia ya 'kubebwa'.

Kwa waamuzi kufanya kazi yao kwa weledi, itamsaidia pia Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa (Taifa Stars), Etienne Ndayiragije katika maandalizi ya kikosi chake kitakachoshiriki kwenye fainali za Kombe la Mataifa ya Afrika kwa Wachezaji wa Ndani (CHAN), ambazo zitafanyika Januari, mwakani huko Cameroon.

Ligi hiyo ndiyo pekee itakayotoa wachezaji wengi watakaounda kikosi kitakachokwenda kupeperusha bendera ya nchi kwenye fainali hizo za CHAN, hivyo wanahitaji kupata misingi imara kuanzia kwenye mazoezi hadi wanapokuwa uwanjani.

Haipendezi kuona waamuzi wanaendelea kufungiwa, huku timu iliyonyimwa haki yake ikiendelea kuumia kwa sababu matokeo ya uwanjani hubaki vile vile.

Nipashe inawakumbusha pia mashabiki wa soka kufahamu mipaka ya majukumu yao na kuacha kuingia mambo ya kiufundi yanayofanywa na makocha.

Nipashe hutolewa na kuchapishwa na:
**THE GUARDIAN LIMITED**

**Mhariri Mtendaji:** Beatrice Bandawe
**Meneja Usambazaji na Masoko:** Emmanuel Lyimo, 0716 500500
**Mapokezi:** 0745 700710
**Matangazo:** 0782 253676
Baruapepe: advertise@guardian.co.tz
**Website:** www.ippmedia.com
epaper.ippmedia.com




## Muungwana Lazima Nilonge

# Umbea wa Simba, Yanga



Na Barnabas Maro

**'UMBEA'** ni tabia ya kutoa habari bila kutumwa au kuulizwa; udaku, udakuzi. Tabia ya kufuatilia au kusikiliza habari za watu wengine bila kutumwa.

'Siri' ni jambo lililo moyoni mwa mtu ambalo mwingine halioni ila yeye mwenyewe. Ni jambo au tukio ambalo bado halijatakiwa kudhihirishwa. Jambo ambalo watu wengi hawalijui, jambo lililofichika.

Mtu anayetarajia kuposa*, hapigi mbiu (pembe inayopulizwa ili kuwaarifu watu jambo fulani; ujumbe au taarifa inayotolewa na mpuliza pembe hiyo).

*Posa ni maombi ya kutaka kuoa yanayopelekwa kwa wazazi wa binti anayehitajika kuolewa; taarifa au ombi la kutaka kumwoa binti kwa wazazi wake; chumbia.

Usajili wa wachezaji, hasa kwa Simba na Yanga, hufanywa bila kificho na kusababisha kile kiitwacho "mwenye kisu kikali ndiye alaye nyama." Kwamba anayekishika kisu kikali ndiye anayeweza kuikata nyama vizuri.

Simba na Yanga hawana siri ila umbea ndio unaotawala wakati wanapohaha kupata wachezaji wa kuwasajili.

Ndo maana ilisemwa: "Siri ya mtungi iulize kata." Maana yake siri ya mtungi wa maji inajulikana na kata ya maji, maana vitu hivi vinatumika pamoja, haviachani.

Methali hii hutumika kwa maana ya kuwa ukitaka kuijua, kwa mfano, siri ya marafiki wawili, mpate mmoja kati yao umwulize, ndiyo atajua, maana wako pamoja kama vile mtungi na kata.

Linapokuja suala la usajili wa wachezaji, lazima Simba na Yanga zitaingiliana, ama kwa dhati (umakini wa moyo) au kuchafuana ili mojawapo, au zote zimkose mchezaji anayegombewa!

Tabia hii imekuwapo kwa miaka mingi kila upande ukiutega mwingine. Huandika mara kwa mara kwamba kisemwacho kuwa Simba na Yanga ni 'watani wa jadi' si kweli kwani watani wa jadi husaidiana katika mambo mbalimbali mmoja anapokuwa kwenye matatizo.

Nyang'anya' ni kitendo cha kuchukua kitu bila ridhaa ya mwenyewe; pora, nyakua. 'Nyang'anyiana' ni kitendo cha kugawana kitu bila ya mpango kwa namna ambayo kila mmoja anataka apate zaidi kuliko mwingine; nyanyia, yaani pata kitu kwa ujanjaujanja, laghai ili kupata kitu.

'Uongozi' ni dhamana ya kusimamia jambo kwenye taasisi au penginepo. Madaraka anayopewa mtu ya kusimamia au kuongoza shughuli.

Hutunduwaa (shangaa, baki kimya bila kutenda jambo au kwa ajili ya kufikiria jambo linalostaajabisha; duwaa) nisikiapo viongozi wa Simba na Yanga wakivutana kuhusu mchezaji fulani anayetakiwa na kila upande!

Kwa nini viongozi wa vilabu hivyo kongwe hawafanyi usajili wao kimya kimya bila kueleza hadharani mchezaji wanaomkusudia au wanaofanya mazungumzo naye ili wamsajili?

Kwa nini huingiliana na hata kuibiana wachezaji kama upande mmoja ukipata tetesi kuwa mchezaji huyo anatakiwa Msimbazi au Jangwani? Huo si 'utani wa jadi' bali ni 'chuki za jadi.' Anayebisha abishe, lakini ukweli ni huo ingawa unaumiza.

Ukichunguza sana utagundua kuwa viongozi wa Simba na Yanga hutaka kuoneshana nguvu ya fedha ilhali hawana uwezo huo!

Wakati Simba wakimtegemea sana MO Dewji kwa kila jambo, Yanga nao wanaitegemea mno Kampuni ya GSM kwa kila kitu baada ya aliyekuwa mfadhili wao wa zamani mambo yake kwenda msobemsobe.

Yanga na Simba zilikuwa moja mwaka 1935 lakini mwaka uliofuatia, (1936) kukawa na mfarakano (hali ya kutoelewana) baina yao. Simba ya sasa ikaitwa Sunderland ambayo ndio hii inayoitwa Simba leo.

Tangu wakati huo, si Yanga wala Simba inayojitegemea yenyewe. Simba ilikuwa ikiwategemea Waarabu ilhali Yanga ikiwategemea Wahindi. Hebu fikiri kwa miaka 85 vilabu hivyo vinavyoitwa 'watani wa jadi' havijaweza kujitegemea ila vinaendelea kuwa tegemezi (-enye kutumainia kiumbe kingine kwa mahitaji yake)!

Je, ni 'watani wa jadi' kweli au 'wajinga wa jadi'? Wana dhamira (nia ya kufanya jambo; azma, kusudio) ya kuviendeleza vilabu hivyo au ni kile kisemwacho 'kupiga pesa'?

Leo, kwa mfano, Mo Dewji (Simba) na GSM (Yanga) wakijitoa, timu hizi zitakuwaje? Viongozi wa vilabu wanaweza kueleza walivyozisaidia timu zao na kuwaletea maendeleo yoyote? Ni yale wasemayo Waingereza: "be coining/minting money" yaani kutajirika haraka haraka!

Ile nyumba ya Yanga pale Jangwani na Simba pale Msimbazi hata kupakwa rangi ni mpaka wadhamini wajitolee! Ukibebwa usilevyelevye miguu, chambilecho wahenga.

marobarnabas@yahoo.com
0784 334 096

# Uuzaji hisa DSE sasa kwa simu

**Na Beatrice Moses**

SOKO la Hisa la Dar es Salaam (DSE), linatarajiwa kuongeza idadi ya wanahisa baada ya kuzindua mfumo mpya wa uuzaji hisa, kupitia simu za mkononi.

Mfumo huo unaotajwa kwa jina la 'Hisa Kiganjani' ulizinduliwa jana jijini Dar es Salaam, unatarajiwa kuongeza idadi ya wawekezaji 550,000 waliopo sasa.

Akizungumza jana kuhusu mfumo huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa DSE, Moremi Marwa, alisema mfumo huo utarahisisha wawekezaji kujiunga na kununua hisa bila kuhudhuria kwenye eneo la soko.

"Mfumo huo unatoa nafasi wa DSE kujitanua kutoka Dar es Salaam kufika kwenye maeneo mengine ya nchi kupitia simu ya mkononi, tunaamini itatoa fursa kwa watu wengi wafanyabiashara na wajasiriamali kujiunga, hivyo kujiongezea kipato," alisema Marwa.

Alisema kufanikiwa kuanza kutumika kwa mfumo huo kumehusisha taasisi kadhaa ikiwamo, Mamlaka ya Vitambulisho vya Taifa (NIDA) na Mfumo wa Malipo ya Kielektroniki Serikalini (GePG).

Akizindua mfumo huo, Ofisa Mtendaji Mkuu wa Mamlaka ya Masoko ya Mitaji na Dhamana (CMSA), Nicodemus Mkama, alisema uwapo wa mfumo huo unatarajiwa kuleta matokeo chanya katika kujenga sekta jumuishi ya fedha.

Alisema mfumo huo unaweza kuwavutia wananchi wanaotumia simu za mkononi ambao kwa takwimu zilizotolewa na Mamlaka ya Mawasiliano Tanzania (TCRA) kwa kipindi kilichoishia Septemba mwaka huu, Watanzania milioni 49.2 wanatumia simu, kati yao milioni 30.5 wanatumia huduma za fedha kwa njia ya simu.

"Mfumo huo unatarajia kuwezesha kuongezeka kwa miamala katika soko la hisa, inatarajiwa ukwasi wa soko la hisa utaongezeka, ni kiashiria muhimu cha ubora wa soko kinachovutia wawekezaji wengi wa ndani na wa kimataifa," alisema Mkama.

Alisema mfumo huo umeidhinishwa baada ya CMSA kujiridhisha kuwa unakidhi matakwa ya sheria, ni salama kwa wawekezaji.

Mkama alisema CMSA itaendelea kujenga mazingira wezeshi na shirikishi kwa lengo la kuhakikisha maendeleo ya masoko ya mitaji yatapatikana, hivyo kuchochea ukuaji wa uchumi nchini.




Mkuu wa Mkoa wa Rukwa, Joachim Wangabo, akipunga mkono baada ya kuliwasha trekta kuashiria uzinduzi wa msimu wa kilimo pamoja na kufungua matumizi ya zana bora za kisasa za kilimo wakati wa hafla iliyofanyika katika Kata ya Ntendo, Manispaa ya Sumbawanga juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Warioba apongeza SUA kwa ubunifu

**Na Frank Kaundula,** MOROGORO

MKUU wa Chuo Kikuu cha Sokoine cha Kilimo (SUA), Jaji Joseph Warioba, ameeleza kuridhishwa na hatua zinazochukuliwa na watendaji wa chuo hicho katika kuimarisha miundombinu ya ufundishaji na utafiti.

Pia amewataka kuongeza bidii katika kusaidia jamii inayowazunguka kupitia utafiti wanaofanya.

Jaji Warioba alisema juzi kuwa jitihada zinazofanywa na SUA katika uanzishaji wa mashamba darasa na kituo atamizi cha kufundisha mbinu za kilimo biashara kwa kutoa mafunzo, zimesaidi kwa kiasi kikubwa kupunguza ya ajira kwa vijana.

Alisema shamba darasa la SUA limeonyesha mafanikio makubwa kwa kuwa mbali na kuzalisha lakini imekuwa sehemu ambayo wanafunzi wanajifunza kwa vitendo kulima na kuhudumia mazao mbalimbali ya kilimo, ufugaji na uvuvi.

"Niseme kuwa mafunzo yale yanayofanywa katika shamba darasa na kituo atamizi ile ni mbegu nzuri sana si kusaidia vijana tu lakini kubadili kilimo chetu kwa sababu watakwenda pale na kujifunza kilimo lakini pia biashara. Kama kweli tunataka kuondoa umaskini ni lazima tufanye hali ya mkulima mdogo iwe na tija zaidi," alisema.

Pamoja na kuwapo kwa matatizo ya rasilimali mbalimbali, alisema chuo kimejitahidi kuhakikisha kinakuwa katika hali ya usafi na ukarabati unafanyika katika majengo na barabara.

Jaji Mkuu Mstaafu, Chande Othman, ambaye Mwenyekiti wa Baraza la SUA, alisema zaidi ya Sh. bilioni 21 zimetumika katika mpango mkakati wa chuo wa awamu ya nne ambao ulianza mwaka 2016 na unatarajiwa kukamilika mwaka 2021. Utekelezaji wake umefikia asilimia zaidi ya 74.

"Kuna mazuri mengi ambayo tumefanya lakini kuna ambayo tunatakiwa kujitahidi. Moja ni suala la jinsia lakini pia kuna hatua chuo kimepiga katika ugani," alisema.

Naye Makamu wa Mkuu wa Chuo, Prof. Raphael Chibunda, alisema katika kuhakikisha chuo hicho kinapanua huduma zake nchini, wameanzisha kampasi katika mkoa wa Katavi inayojulikana kama Kampasi ya Mizengo Pinda

Alisema kuanzia mwaka huu wa masomo, kampasi hiyo itatoa programu tatu ambazo ni shahada ya utunzaji wa rasilimali nyuki, astashada ya kilimo pamoja na mafunzo katika ngazi ya cheti ya kuongoza watalii na uwindaji.

"Ili kufundisha vizuri tumeshafanya uamuzi kuwa sasa kufundisha kwa nadharia tu hivyo tutafundisha zaidi kwa vitendo kwa hiyo tumeshapeleka trekta, trela pamoja na opareta kwa ajili ya kufungua shamba la mafunzo katika kampasi hiyo.

"Lakini pia tumemaliza ujenzi wa shamba darasa la nyuki na tayari tuna mizinga 70 ambayo ina nyuki. Kwa hiyo wanafunzi wanapoanza mwaka huu, watatumia mashamba hayo kujifunzia," alisema Prof. Chibunda.

# Ofisa afya kortini tuhuma za rushwa

**Na Hamisi Nasri,** Masasi

TAASISI ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa (TAKUKURU) Masasi mkoani Mtwara, imempandisha kizimbani katika Mahakama ya Wilaya ya Masasi, Ofisa Afya wa Hospitali ya Wilaya ya Mkomaindo, Christopher Ponela (28) kwa tuhuma ya kuomba na kupokea rushwa.

Mshtakiwa huyo alifikishwa mahakamani hapo juzi mbele ya Hakimu Mkazi Shaibu Mzendeh, akikabiliwa na mashtaka manne ya kushawishi kupewa Sh. 300, 000, kupokea Sh. 50,000 na kukamatwa na rushwa ya Sh. 200,000.

Mwendesha Mashtaka wa TAKUKURU, Charles Mtungila, alidai mahakamani hapo kuwa Ponela ambaye ni mtumishi wa Halmashauri ya Mji Masasi katika Hospitali ya Mkomaindo, amefikishwa kwa kwenda kinyume cha kifungu cha 15 cha ya Sheria ya Kuzuia na Kupambana na Rushwa namba 11 ya mwaka 2007 baada ya kuomba rushwa.

Alidai kuwa Novemba 10, mwaka huu, maeneo ya Migongo mjini Masasi, mshtakiwa alikwenda kufanya ukaguzi wa mazingira ya kiafya katika nyumba ya kulala wageni inayomilikwa na John Milanzi (73).

Baada ya mshtakiwa huyo kufanya ukaguzi, alidai kuwa alibaini makosa ya kiafya ambayo mmiliki wa nyumba hiyo alikuwa ameyakiuka.

Mtingula alidai kuwa mshtakiwa baada ya kubaini makosa hayo, aliamua kumwandikia faini na kumtaka Milanzi kulipa Sh. Milioni moja ili kurekebisha kasoro ambazo zimebainika kwenye nyumba hiyo.

Baada ya kumtaka mmiliki huyo kulipa fedha hizo, ofisa huyo alirudi siku iliyofuata na kumshawishi kutoa rushwa ya Sh. 300,000 ili kumsamehe na kufuta kasoro zilizobainika.

Mwendesha mashtaka alidai kuwa ofisa huyo alimshawishi Milanzi kutoa Sh. 50,000 ikiwa kama sehemu ya Sh.300, 000 aliyokuwa ameiomba na alipatiwa huku akiambiwa arudi siku inayofuata kuchukua kiasi kilichobaki.

Kutokana na ahadi hiyo, alidai kuwa Novemba 14, maeneo ya Hospitali ya Mkomaindo, maofisa wa TAKUKURU waliweka mtego baada ya kupata taarifa kutoka kwa msiri wao na kumkamata ofisa huyo akiwa na Sh. 200,000 alizokuwa amepewa na Milanzi kwa lengo la kumfutia makosa yake.

Mshtakiwa alikana mashtaka yanayomkabili na alipewa dhamana baada ya kutimiza masharti ambayo ni kuwa na wadhamini wawili ambao ni watumishi wa serikali watakaotia saini fungu la dhamana la Sh. milioni mbili kila mmoja.

Kesi hiyo imeahirishwa hadi Desemba Mosi, mwaka huu kwa upande wa mashtaka kutoa ushahidi wa tukio hilo.

# RAS awataka wahitimu misitu kujituma

**Na Francis Godwin,** IRINGA

KATIBU Tawala wa Mkoa wa Iringa, Hapinnes Seneda, amewataka wahitimu wa Chuo cha Viwanda vya Misitu (FITI), kuhakikisha wanajituma zaidi katika utendaji kazi ili kuongeza thamani ya mazao ya misitu kwa kuzalisha samani zenye ubora.

Kwa kufanya hivyo, Seneda amesema taifa litaachana na utegemezi wa samani kutoka nje ya nchi. Akizungumza juzi na wahitimu wa FITI na uongozi wa Taasisi ya Uendelezaji Misitu Tanzania (FDT), Seneda alisema serikali imeendelea kuboresha mazingira ya uwekezaji wa viwanda mbalimbali vikiwamo vya uchakataji wa mazao ya misitu, hivyo kupitia chuo hicho, ni wazi watapatikana wataalamu zaidi wa kuongeza thamani ya mazao ya misitu.

Seneda alisema Iringa ni moja ya mikoa yenye utajiri mkubwa wa miti, hivyo iwapo wahitimu hao watajituma katika kutumia elimu waliyopata kwa kujitika zaidi katika kuongeza thamani ya mazao ya misitu kwa kutengeneza samani zenye ubora, ni wazi soko la bidhaa zao litaongezeka zaidi.

Aliwataka wahitimu hao kwenda kufanya kazi kwa bidii na kuachana na tabia ya kutanguliza maslahi zaidi badala ya kuonyesha ubora wa kazi katika maeneo ambayo wanakwenda kufanya kazi kwa kujitolea.

Kupitia mafunzo ambayo wamepata, alisema wahitimu hao wana uwezo mkubwa wa kuongeza ujuzi katika kazi ili kutengeneza bidhaa za kisasa zitokanazo na mazao ya misitu.

Kwa mujibu wa Katibu Tawala, sababu ya watu kukimbilia kununua bidhaa za nje ni ubora uliopo kwenye bidhaa hizo lakini kama vijana na wawekezaji wa ndani wataboresha bidhaa zao, hakutakuwa na ulazima wa kuagiza samani kutoka nje.

Alisema serikali imekuwa ikitoa mikopo kwa vijana kupitia Halmashauri ili kuwawezesha wale waliojiunga katika makundi kuongeza mitaji katika shughuli zao japo si rahisi kwa serikali kutoa mikopo kwa watu ambao hawaonyeshi wanafanya nini.

Pia alisema hata kupitia taasisi za kifedha, mikopo ipo lakini lazima kuwapo na andiko kutoka kwa waombaji ambalo linaonyesha shughuli wanayofanya au wanayotaka kufanya.

Seneda aliipongeza FDT kwa jitihada mbali mbali inazoendelea kufanya katika mkoa wa Iringa kuona mazingira yanaendelea kuboreshwa kwa kupanda miti zaidi pia kuonyesha fursa zitokanazo na mazao ya misitu katika kuwakomboa wananchi wengi hasa wale wanaojishughulisha na kilimo cha miti .

Mkurugenzi Mtendaji wa FDT, David Shambwe, alisema ofisi yake imeendelea kupata ushirikiano mkubwa kutoka ofisi ya mkuu wa mkoa na tayari wamezungumza na wenye viwanda vya mazao ya miti na kupeana elimu mbalimbali .

Shambwe alisema programu hiyo ni moja ya chachu kubwa kwa vijana na uendelezaji wa viwanda vyenye ubora nchini hasa katika mazao ya misit -*-u iwapo wadau mbalimbali wataunga mkono .




Katibu Mkuu Wizara ya Ujenzi, Uchukuzi na Mawasiliano, Elius Mwakalinga (aliyenyoosha mkono), akimsikiliza Ofisa Mauzo na Masoko wa kampuni ya GF Trucks & Equipment's Ltd, Juma Lukolo (kulia), wakati wa ufunguzi wa maonyesho ya mkutano wa Chama cha Wakandarasi Wazalendo na Wadau wa Ujenzi nchini, jijini Dar es Salaam juzi. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# Utafiti: Wengi hawajui kama wana matatizo ya meno

**Na Neema Emmanuel,** MWANZA

UTAFITI wa kitalaam unaonyesha kwamba wananchi wengi wana matatizo ya kinywa na meno licha ya kuwa wenyewe hawajui.

Hayo yamebainishwa juzi na daktari bingwa wa upasuaji wa shingo, kichwa na meno kutoka Hospitali ya Rufani ya Kanda ya Bugando, Dk. Emmanuel Motega.

Dk. Motega alisema utafiti uliofanyika unaonyesha kuwa asilimia kubwa ya wananchi wana matatizo ya kinywa na meno na kwamba wanaishi na matatizo hayo.

Sababu kubwa, kwa mujibu wa daktari bingwa huyo, ni kuwapo kwa uelewa mdogo juu ya magonjwa hayo huku akiwaomba wananchi wanapohisi maumivu ya meno, harufu mbaya ya kinywa, kuwahi hospitalini.

Alisema mtu akichelewa kupata matibabu, bakteria huingia sehemu zingine za mwili na kusababisha magonjwa mengine kama moyo, majipu ya kashuka kwenye shingo au kifuani, uvimbe na saratani.

"Kwa sasa huduma ya meno imeboreshwa kwa kiwango cha hali ya juu kwani tunaweza kutibu jino bila kung'oa. Tunaweza kuziba meno, kusafisha fizi ambazo zimepata magonjwa, kufanya upasuaji wa shingo na kichwa," alisema Dk. Motega.

# TARI yakunwa utekelezaji agizo la JPM

**Na Ashton Balaigwa,** SINGIDA

WAJUMBE wa Bodi ya Taasisi ya Utafiti wa Kilimo Tanzania (TARI), wameridhishwa na utekelezaji wa majukumu ya watafiti na watendaji yaliyotolewa na Rais John Magufuli, katika uendelezaji wa zao la korosho nchini.

Mwenyekiti wa Bodi ya TARI, Dk.Yohana Budeba, aliyasema hayo baada ya kutembelea mashamba mapya ya korosho katika Wilaya ya Manyoni mkoani Singida.

Dk. Budeba alisema maagizo ya serikali yaliyotolewa ya kupanua kilimo cha korosho kwenye mikoa mipya, utekelezaji wake umeshaanza kwa kasi kwenye mikoa ambayo ilikuwa hailimi zao hilo.

Alisema utekelezaji huo umeshaanza kwenye mikoa ya Dodoma, Morogoro, Iringa, Singida, Tabora, Katavi, Songwe, Kigoma , Kilimanjaro, Mbeya, Njombe na Ruvuma, kwamba tayari wananchi wamepewa elimu ya zao hilo, pamoja na kuanzisha vitalu vya uzalishaji wa miche ya korosho.

"Sisi kama bodi tumeridhishwa sana na watafiti namna walivyotekeleza agizo la Rais Magufuli katika kuinua kilimo cha korosho kwenye mikoa mipya," alisema Dk. Budeba.

Mmoja wa wajumbe wa bodi hiyo, ambaye ni Mkurugenzi Mtendaji wa Mtandao wa Vikundi Vidogo vya Wakulima Tanzania (Mviwata), Stephen Ruvuga, alisema utekelezaji wa agizo Rais Magufuli utaifanya nchi kuinuka kiuchumi.

Mjumbe mwingine wa bodi hiyo, Dk. Erick Shirima, alitaka watafiti hao kuendelea kuzalisha kwa wingi mbegu za korosho, kutokana na wakulima wengi kuitikia wito wa kulima zao hilo.

Mkurugenzi Mkuu wa TARI, Dk. Geofrey Mkamilo, alisema katika kutekeleza maagizo ya Rais Magufuli, wameweka mkakati wa kuongeza uzalishaji wa korosho kutoka tani 315,000 za sasa, hadi tani milioni moja ifikapo mwaka 2023.

Mwenyekiti wa wakulima wa korosho katika Wilaya ya Manyoni, Issa Madenge, alishukuru serikali kwa kuamua kuendeleza zao hilo kwa mikoa ambayo haikuwa inalima korosho, akisema itasaidia kuwainua kiuchumi wakulima.

# Maambukizi VVU yawatikisa vijana

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

IMEELEZWA kuwa zaidi ya asilimia 50 ya maambukizi mapya ya virusi vya UKIMWI nchini yapo kwa kundi la vijana wenye umri kati ya miaka 15 hadi 35.

Akizungumza na waandishi wa habari jana jijini hapa, kuhusiana na maadhimisho ya Siku ya Ukimwi Duniani, Katibu Mkuu, Ofisi ya Waziri Mkuu Sera, Uratibu na Uwekezaji, Dorothy Mwaluko, alisema umri huo ni kwa mujibu wa Sera ya Vijana ya mwaka 2007.

Alisema maambukizi mapya nchini bado ni tishio, hivyo kuna wajibu wa kutekeleza mikakati yote ya kuhakikisha yanatoweka.

"Takwimu zinaonyesha watu takribani 72,000 wanapata maambukizi mapya kwa mwaka, hiyo ina maana kuwa kwa mwezi watu 6,000, watu 200 hupata kwa siku na kwa saa moja ni watu wanane.

"Kwa takwimu hizi ni lazima tutekeleze mikakati kwa namna mbili, moja kwa kundi lililoambukizwa kwa kuzingatia 90 tatu ili wafubaze virusi na kuendelea kufanya kazi kwani mtaji wa maskini ni nguvu na sio virusi,"alisema.

Alitaja kundi la pili la kuliwekea mikakati ni la wale wasioambukizwa kwa kuweka jitihada ili wasiambukizwe.

"Ili vijana wetu wasiambukizwe ni lazima vijana waongozwe na kauli ya kusema,mwili wake wa huyo kijana ndio maisha yake na maisha yake ndio nguvu ya ujenzi wa taifa lake," alisisitiza.

Kuhusu maadhimisho ya siku hiyo, Mwaluko alisema kitaifa yatafanyika mji wa Moshi mkoani Kilimanjaro kuanzia Novemba 25 siku ambayo itazinduliwa rasmi kwa kufanya matembezo ya hisani kwa ajili ya kutangaza na kuhamasisha uchangiaji wa mfuko wa UKIMWI (AIDS Trust Fund).

Pia alisema kuanzia Novemba 25 hadi Disemba Mosi, kutakuwa na maonyesho ya shughuli za wadau wa kudhibiti UKIMWI na virusi vya UKIWMI nchini yakijumuisha na utoaji wa elimu mbalimbali katika viwanja vya Mandela.

Alisema Novemba 26 na 27 kutakuwa na kongamano la kisayansi la kitaifa la kutathimini hali na mwelekeo wa udhibiti wa virusi vya UKIMWI na UKIMWI ikifuatiwa na mdahalo wa vijana Novemba 28 kwa ajili ya kuzungumzia masuala mbalimbali yanayohusiana na afua ya UKIMWI na Virusi vya UKIMWI.

**Takwimu zinaonyesha watu takribani 72,000 wanapata maambukizi mapya kwa mwaka, hiyo ina maana kuwa kwa mwezi watu 6,000, watu 200 hupata kwa siku na kwa saa moja ni watu wanane.**

# Wataka mabadiliko sheria ya ndoa

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

JUKWAA la Utu wa Mtoto (CDF), limeomba serikali kufanyia marekebisho sheria zote kandamizi kwa mtoto wa kike ikiwamo Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971.

Ofisa Mawasiliano wa CDF, Celina Baragwiha, alitoa ombi hilo jana jijini hapa kwenye mafunzo ya siku mbili yaliyoandaliwa na jukwaa hilo kwa kushirikiana na Taasisi ya Equality Now ya kuwajengea uwezo wadau wa elimu Tanzania kuwa na uelewa wa sheria na sera kandamizi dhidi ya mtoto wa kike.

Alisema mtoto wa kike bado anakandamizwa na sheria na zinakinzana na Katiba ya Nchi, hivyo zikifanyiwa marekebisho zitatoa fursa ya kufikia ndoto zake kielimu.

"Sheria ya Ndoa ya Mwaka 1971 kifungu cha 13 na 17 kinaruhusu mtoto wa miaka 14 kuolewa huku wazazi na mahakama wakiruhusu. Sheria ya Elimu inamruhusu asome, Sheria ya Mtoto inamlinda mtoto asome," alisema.

Pamoja na hayo, alisema bado kuna mila na desturi ambazo zinakinzana na sheria na zinamkandamiza mwanamke.

Alisema jukwaa hilo limekuwa likitoa elimu kwa jamii ili kuondokana na vitendo vinavyomkosesha haki ya kupata elimu mtoto wa kike.

"Tunafanya kazi wilaya tatu ikiwamo Ilala ambako kuna vitendo vya ukeketaji, watu wanatoka Tarime kwenda Kitunda Ilala kufanya vitendo hivyo, kutokana na Tarime kuwapo na udhibiti mkubwa, pia tunafanya kazi wilaya ya Tarime ambako ndoa za utotoni na ukeketaji ni mkubwa," alisema.


Akizungumzia kuhusu maadhimisho ya Siku 16 za Kupinga Ukatili wa Kijinsia, Ofisa huyo alisema siku hizo jukwaa hilo litatumia kupinga ukatili wa kingono kwa kwenda kwenye vyuo mbalimbali kwa kujadiliana na wanafunzi wa jinsia zote.

Naye Ofisa Mtetezi kutoka Mtandao wa Elimu Tanzania, Nasra Kibukila, alisema watoto wa kike wengi kwa sasa wamepewa fursa ya kupata elimu na mpango wa serikali wa elimu bila malipo jambo ambalo limeongeza udahili wao shuleni.

Pia alisema mkakati wa serikali kuwa na shule moja ya wasichana kila mkoa kwa ajili ya wanafunzi wa kike wa masomo ya sayansi itasaidia kuwapo mwamko wa watoto hao kusoma sayansi.

Sambamba na hilo, aliomba serikali kuangalia sheria zinazomkandamiza mtoto wa kike na kuzifanyia marekebisho ili wafikie ndoto zao.

"Kulingana na hii sheria ya ndoa tunaona mtoto wa kike anatakiwa kuolewa akiwa na umri wa miaka 15 wakati mtoto wa kiume anaoa akiwa na miaka 18,"alisema.



Ofisa Mipango wa Jiji la Dodoma, Rozalia Hhari, akizungumza na washiriki wa mafunzo ya asasi ya kiraia kuhusu ushawishi na utetezi wa watu wenye ulemavu, jijini Dodoma jana. **PICHA: PETER MKWAVILA**

# TAMISEMI yajivunia kupungua utapeli

**Na Augusta Njoji,** DODOMA

OFISI ya Rais, Tawala za Mikoa na Serikali za Mitaa (TAMISEMI), imesema kuanzishwa kwa kituo cha huduma kwa wateja katika ofisi hiyo kumepunguza matukio ya utapeli, huku watumishi wakiagizwa kushughulikia kero ndani ya siku tatu na si zaidi.

Katibu Mkuu wa Ofisi hiyo, Joseph Nyamhanga, aliyasema hayo jana alipotembelea kituo hicho kilichoanzishwa Agosti 6, mwaka huu.

Alisema kabla ya kuanzishwa kwa kituo hicho, kulikuwa na matukio mengi ya utapeli hususani kwa walimu wanaofuatilia uhamisho ikiwamo kutolewa kwa barua feki za uhamisho.

"Watumishi wengi wetu ni walimu na hawa ndio walikuwa waathirika wakubwa wa tatizo hili na ilifikia hadi kugushiwa barua za uhamisho ambazo walikuwa wakizigharamia, lakini kwa sasa hali hiyo haipo," alisema.

Aidha, Nyamhanga aliagiza wakuu wa idara za wizara hiyo kushughulikia kero na hoja za wateja wa wizara hiyo ndani ya siku tatu na si zaidi ya hapo.

Alitoa rai kwa watumishi na Watanzania kwa ujumla kutumia kituo hicho jambo ambalo litasaidia kuwaondolea kero ya kusafiri na gharama.

Msimamizi wa Kituo cha Huduma kwa Wateja, Antelma Mtemahanji, alisema ndani ya miezi minne tangu kuanzishwa kwa kituo hicho, hoja na matatizo ya wateja yameshughulikiwa kwa asilimia 99 huku asilimia moja ikiwa katika hatua za kushughulikiwa.

Alisema tangu kuanza kituo hicho, wamepokea simu 15,886, wateja waliosajiliwa ni 5,571 na hoja zilizosajiliwa ni 5,571.

Mtemahanji alisema kabla ya kuanzishwa kwa kituo, walikuwa wanapokea wageni wenye shida mbalimbali kutoka watu 87 hadi 129 kwa siku lakini kwa sasa idadi hiyo imepungua na hawazidi watu 20.

Alisema baadhi ya hoja ambazo zimeshughulikiwa ni uhamisho kwa walimu, stahiki za watumishi ikiwa ni kupanda daraja au kubadilishiwa mshahara na kutaka kupata ufafanuzi wa mifumo na ajira.

## HABARI ZANZIBAR

## Watakiwa kuzingatia mafunzo ya takwimu

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

WASHIRIKI wa Mafunzo ya Ukusanyaji wa Takwimu Sahihi wametakiwa kuhakikisha mafunzo waliyopatiwa juu ya ukusanyaji wa taarifa kuyafanyia kazi ili kufanikisha lengo lililokusudiwa.

Mkurugenzi Mipango Sera na Utafiti katika Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali, Khalid Masoud Waziri, alisema hayo jana alipokuwa akifunga mafunzo ya ukusanyaji wa takwimu sahihi za maji safi na salama, usafi wa mwili na mazingira katika shule, kwenye ukumbi wa Taasisi ya Sayansi na Teknolojia Karume, Mbweni mjini Unguja.

Alisema lengo ni kupeana taaluma ili kuwaelimisha na wengine namna ya ukusanyaji wa takwimu ili kuisaidia serikali katika kutatua changamoto mbalimbali na kupanga mipango yake ya maendeleo kwa urahisi.

Alisema katika ukusanyaji wa taarifa maandalizi mbalimbali yanahitajika na kumekuwapo matatizo mengi ya kimakosa ambayo yanafanya taarifa zinazokusanywa kuwapo na makosa na hivyo kufanya mipango iliyokusudiwa kutofikiwa.

Khalid aliwataka washiriki hao kutambua kuwa wana mchango mkubwa kwa serikali katika kuhakikisha wanatoa elimu inayostahili kwa walimu kuhusu ukusanyaji wa takwimu sahihi katika jamii.

Pia alilishukuru Shirika la Umoja wa Mataifa la Kuhudumia Watoto (UNICEF) kwa uamuzi wa kutoa mafunzo hayo kwa wataalamu wa takwimu kutoka taasisi mbalimbali ili kuleta maendeleo ya elimu nchini.

Naye Ofisa Maji na Usafi wa Mazingira kutoka UNICEF Kanda ya Dar es Salaam, John Mfungo, aliesema dodoso ambalo linatumika katika kukusanya takwimu, imeonekana kuwa na upungufu katika ukusanyaji wa takwimu sahihi za matumizi ya maji safi na salama, usafi wa mwili na mazingira ndiyo maana wameandaa mafunzo hayo.

Mafunzo hayo yamewashirikisha watendaji mbalimbali kutoka mabaraza ya miji, manispaa, Wizara ya Afya, Ofisi ya Mtakwimu Mkuu na yameandaliwa na UNICEF kwa kushirikinana na Wizara ya Elimu na Mafunzo ya Amali.

# Tofauti kisiasa zavunja ndoa Z'bar

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

TOFAUTI za itikadi za kisiasa kwa wanandoa Zanzibar zimesababisha migogoro ya ndoa na baadhi kuvunjika.

Hayo yalielezwa juzi na wanaharakati wa kutetea haki za wanawake na watoto katika mkutano baina ya viongozi wa dini na waharakati kutoka asasi za kiraia, ulioandaliwa na Chama cha Waandishi wa Habari Wanawake Tanzania (TAMWA) ofisi za Zanzibar uliofanyika mjini hapa.

Walisema katika harakati za uchaguzi mkuu wa Oktoba, mwaka huu, baadhi ya ndoa zimetetereka na baadhi kuvunjika kutokana na itikadi za kisiasa kwa wanandoa.

Kiongozi wa Dini ya Kiislamu, Sheikh Khamis Abdilhamid, alisema kumekuwapo baadhi ya wanandoa kuwalazimisha wake zao kuwachagua viongozi wanaowataka wao kinyume cha sheria ambayo imeweka wazi kuwa kila mtu ana haki ya kumchagua anayempenda.

Alisema mchakato wa kura na uhuru wa kuchagua haukuanza leo bali enzi za mitume, hivyo hakuna kitu kigeni ambacho kingewapa nguvu zaidi wanaume kuwaamulia wake zao jinsi ya kumchagua kiongozi katika uchaguzi.

Sheikh Kamis alisema uhuru wa kuchagua ni haki ambayo ipo katika kila sehemu na hata enzi za Nabii Yunnus alipigiwa kura na kuchaguliwa awe sehemu ya kutoswa baharini na kila mtu aliheshimu uamuzi wa kura hiyo na hakuna mtu aliyelazimishwa kumchagua mwingine baada ya yeye.

Alisema wako baadhi ya wanandoa wamefika mbali zaidi kuwatishia wake zao talaka na wengine wamewahi kuwaacha kabisa kutokana na tofauti za kisiasa.

Kutokana na mazingira hayo, alisema si sahihi kwa wanandoa kutishiana talaka kwa masuala ya kisiasa na kufanya hivyo ni kosa.

"Ni lazima watu wafahamu kuwa si kila talaka hutundikwa kuna mambo mengine mwanamke hawezi kuachika kwa sababu tu mume wake kasema akifanya kitu fulani atakuwa ameachika bila kitu hicho kuwa na msingi,' 'alisema.

Awali, akiwasilisha ripoti ya utekelezaji, Laila Khamis Jumbe kutoka Jumuiya ya Wanasheria Wanawake Zanzibar (ZAFELA), alisema migogoro ya ndoa walikutana nayo katika eneo la kusini Unguja pamoja na baadhi ya maeneo katika Wilaya ya Kati.

Alisema baadhi ya wanaume katika ndoa wamekuwa wakiwalazimisha wake zao kuwachagua viongozi wale wanaowapenda wao na sio kutoa fursa kwa mwanamke kumchagua kiongozi anaempenda yeye.

Laila alisema katika uchaguzi mkuu uliopita yamejitokeza baadhi ya matukio ikiwamo baadhi ya wanaume huwaongoza wake zao hadi vituo vya kupigia kura na kuwapa amri kuchagua kiongozi ambaye (mwanamume) anamuunga mkono.



Mkurugenzi wa Taasisi ya Uvuvi Zanzibar, Zahor Kassim, akizungumza kuhusu kuanzishwa kwa Wizara mpya ya Uchumi wa Buluu na Uvuvi, ofisini kwake eneo la Darajani, mjini Zanzibar jana. **PICHA: RAHMA SULEIMAN**

# Uturuki yapongezwa kusaidia yatima

**Na Rahma Suleiman,** ZANZIBAR

MLEZI wa Jumuiya ya Hayrat ya Zanzibar yenye makao makuu nchini Uturuki, Balozi Seif Ali Iddi, ameipongeza taasisi hiyo kwa uamuzi wake wa kuwasaidia watoto yatima wa Zanzibar, kuinua viwango vyao vya elimu vitavyoweza kubadili maisha yao.

Balozi Seif aliyasema hayo jana wakati akizungumza na Makamu wa Rais wa Jumuiya hiyo, Feridun Isikl, nyumbani kwake Kama, Wilaya ya Magharibi 'A', Unguja.

Alisema lengo la jumuiya hiyo la kutaka kuanzisha shule kwa ajili ya watoto yatima Zanzibar ataliunga mkono na litasaidia serikali kukuza kiwango cha elimu kwa watoto hao.

Balozi Iddi alisema ili kupata wataalamu zaidi wa kuzitumikia fani mbalimbali kuijenga nchi yao, ni lazima waandaliwe mazingira mazuri ya elimu na hatua ya jumuiya hiyo kutaka kujenga shule hiyo, itasaidia kuwakomboa watoto wa kundi hilo ambalo mara nyingi linahitaji kupewa msaada.

Alisema jumuiya hiyo inakusudia kujenga shule katika eneo la Panga Tupu, ambayo itakuwa na uwezo wa kuchukua watoto 5,000 ambao asilimia 50 watakuwa yatima na asilimia 50 ni watoto wengine ambao watasoma kwa kulipia gharama kidogo.

Ujenzi wa shule hiyo katika kijiji hicho, alisema utapunguza ukosefu wa huduma muhimu kwa vile tayari serikali inakusudia kujenga kituo cha afya sehemu hiyo.

Alisema inafurahisha kuona kuwa taasisi hiyo tayari imekuwa ikitoa misaada mbalimbali kwa wananchi wa Zanzibar, ikiwamo ya uchimbaji wa visima vya maji safi na salama na utoaji wa sadaka.

Jumuiya hiyo, alisema ana imani kuwa itafanya vizuri katika uwekezaji huo na hivi sasa tayari inatoa huduma katika shule ya kijiji cha kulelea watoto yatima na wanaoishi katika mazingira magumu (SOS), jambo ambalo linaonyesha walivyokubalika kwa wananchi.

Naye Makamu wa Rais wa Jumuiya hiyo, Isikl, akitoa maelezo yake, alisema amefurahishwa na serikali ya Zanzibar, kuamua kushirikiana na taasisi hiyo kwa kuonyesha kuwaunga mkono kuwekeza katika sekta ya elimu.

Alisema wamelazimika kuwasaidia watoto yatima kwa kuwajengea shule hiyo, kwa vile vitabu vya dini ya Kiislamu vimekuwa vikisisitiza suala la kuwatunza kwa kuwapa mahitaji yao ikiwemo elimu huduma ya maji safi na salama.

Makamu huyo wa Rais aisema wanatarajia mradi huo ukianza wahitimu wa shule hiyo watakaofanya vizuri katika masomo yao, watawapa nafasi ya masomo ya juu katika vyuo vikuu vya Uturuki.



**RAHAMA MWANA KULITAFUTA, MWANA KULIPATA** Uk.14

Nipashe MWANGA WA JAMII
BT BURUDANI TELE
JUMAMOSI NOVEMBA 21, 2020



## SWALI GUMU

# Zuchu, Nandy yupi mkali?

SWALI ambalo bado halijapatiwa jibu, huku mjadala mkali ukiendelea katika mitandao ya kijamii kuhusu wasanii hawa wawili wa Bongo Fleva, Nandy na Zuchu, nani mkali zaidi.

Kutokana wanamuziki wote wawili kuonekana kuwa na vipaji vya hali ya juu vya kuimba, mashabiki wa muziki wamegawanyika lakini imekuwa kitendawili kujua yupi yupo juu.

Mwaka 2020 wasanii wote wawili wamefanya vizuri na kila mmoja kukonga mioyo ya mashabiki wao kwa kutoa ngoma kali.

Hata hivyo, Zuchu ameonekana kupata mafanikio kwa haraka zaidi tofauti na Nandy, kwani imemchukua miezi mitano pekee kupata umaarufu nchini na Afria Mashariki.

Vibao vyake vipya kama Cheche, litawachoma na My Number One, alioshirikishwa na Rayvanny, vimefanya vizuri kiasi cha kujizolea wafuasi wengi kila kona.

Nandy kama kawaida yake amejaribu kutoa ladha tofauti kwa kibao chake 'Do Me' ambacho ameimba pamoja na mpenzi wake Billnass na wimbo unaofanya vizuri hivi sasa "Nibakishie' ambao amemshirikisha Ali Kiba.

Hivi karibuni wanamuziki wote wawili wamejikuta wakipata tuzo za Afrimma, wakati Zuchu ameshinda kipengele cha msanii bora anayechipukia, Nandy akishinda msanii bora wa kike Afrika Mashariki.

Kutokana na kazi ya wanamuziki wote wawili imekuwa vigumu kupata jibu kwamba yupi anaweza kuliko mwenzake.

BASI SAWA

## P Funk akumbuka Daz Nundaz

PRODYUZA mkongwe wa muziki wa Bongo Fleva, P Funk Majani, amewashauri wasanii waliokuwa wanaunda kundi la 'Daz Nundaz' Ferooz na Daz Baba kuacha utoto ili kurudisha kundi hilo.

P Funk Majani ametumia ukurasa wake wa mitandao wa kijamii kama Twitter na Instagram, kutoa ujumbe huo baada ya wimbo wa kundi hilo uitwao 'Kamanda' uliotoka mwaka 2001 kufikisha wasikilizaji laki 1 kwenye mtandao wa Boom Play ambao una 'deal' kwa kuuza na kusikiliza nyimbo.

"Ahsanteni kwa support, Ferooz na Daz Baba acheni utoto pigeni kazi ya pamoja mrudishe bendera ya Daznundaz" ameandika.

Kundi hilo lilikuwa lina jumla ya wasanii watano ambao ni Ferooz, Daz Baba, Critic, La Rumba na Sajo.



## Nandy we ni muungwana

MSANII wa muziki wa Bongo Fleva, Nandy, amesema mazito kutokana na wimbo wake mpya aliomshirikisha Ali Kiba, kuendelea kufanya vizuri sokoni.

Bila kuficha, Nandy, amemshukuru Kusah kumtungia mashairi ya wimbo huo, huku akimsifia kwamba amemtendea jambo kubwa katika maisha yake na kamwe hawezi kumsahau.



"Siku uliyonipigia na kuniambia una kitu kizuri juu yangu sikuamini, lakini ulipokuja studio tukakutana kwa mara ya kwanza, hukuchukua hata masaa mawili kumaliza huu wimbo!! Umenipa wimbo mkubwa sana unaweza usione saa hivi ila baada ya mwezi utaniambia!! Na Asante sana sababu matunda nayaona tangu niachie huu wimbo," amesema Nandy kupitia ujumbe alioweka katika ukurasa wake wa Istagram.




# Waluguru kutambulisha wanenguaji wapya

BENDI ya Waluguru Original, imeimarisha safu ya ushambuliaji wa jukwaa kwa kuongeza wanenguaji wapya wakati huu ambao inajiandaa kushuti video ya nyimbo za albamu mpya.

Mkurugenzi wa bendi hiyo, Killer Man amesema wameongeza wanenguaji wawili aliowataja kwa majina ya Happy Gadau na Regina Filbert ambao wamewahi kufanya kazi katika bendi kubwa za jijini Dar es Salaam.

"Wakati tukijiandaa kushuti video ya baadhi ya nyimbo zetu, tumeona tuimarishe kwanza safu ya ushambuliaji wa jukwaa, kwa kuongeza wanenguaji vibonge watakaopamba video yetu," amesema Killer Man.

Amesema, albamu yao inayoitwa 'Kikao cha Wahenga ina nyimbo sita.

# Siri ya mke wangu; unayempenda utamjali

**Na Adam Fungamwango**

MANENO matamu wakati wa kufunga ndoa ambayo wanandoa wote hupenda kuyasikia ni yale yanayosema 'tutaishi kwa shida na raha, hadi kifo kitakapotutenganisha'.

Ni maneno matamu na ya faraja kwa anayetendewa. Lakini nani atatenda? Hapo ndipo kunakuwa ugumu. Lakini si kwa wanandoa tu. Hata wapenzi wa kawaida. Jinsi ya kujua mtu anayekupenda ni kuangalia yule anayejitolea kwa matatizo yote yanayokupata. Mpenzi wa kweli hakupendi wakati wa furaha na raha tu. Hata wakati wa matatizo anakuwa na wewe. Tena anajivisha matatizo yanakuwa kama ya kwake. Ukiwa na mtu kama huyo usimuache, hata kama ana upungufu fulani machache kwa sababu hakuna mwanadamu asiye na upungufu.

Filamu ya 'Siri ya Mke Wangu' inamzungumzia kijana aliyepatwa na matatizo makubwa kwenye ndoa yake. Lakini akapambana na kuyavaa matatizo ya mkewe, badala ya kuamua kumuacha.

Imechezwa na wasanii wengi chipukizi, chini ya msanii mkongwe Muhogo Mchungu.

Sheddy na mkewe Moreen wanaishi kwa amani na utulivu. Lakini kuna mkasa mkubwa unatokea.

Siku moja Moreen anasimamishwa na jamaa njiani akimtongoza. Akamkakaa. Haikusaidia. Hakuwa mtu wa kawaida. Alikuwa jini. Siku moja nyingine akamtokea. Akamkumbuka. Lakini sasa akatumia njia zake za kijini, Moreen akakubali

Uhusiano wa Moreen ulipoanza, ulimletea shida mno Sheddy. Mkewe alibadilika. Wakati mwingine anaporejea, anamkuta mkewe ni kama amemkumbatia mtu na kuwa kwenye hali ya mahaba. Wakati huo anakuwa yuko na jini, lakini yeye hamuoni.

Ikafika wakati jini akamchukua mwanamke huyo na kumpeleka kwao ujinini na kumpa zawadi nyingi ya vito vya dhahabu, marashi na zinginezo. Tabia ya mkewe kubadilika tabia, ilimfanya utendaji wa kazi wa Sheddy kushuka.

Alimua kwenda kwa mganga ili kujua ni mwanamume gani anayemzuzua mkewe. Alichoambiwa na mganga alichoka. Akaambiwa ni jini ndilo linalomzuzua mkewe. Ana uhusiano wa kimapenzi na jini moja hatari. Akapewa dawa kwa ajili ya kumwagia atakapomuona. Alifanya hivyo, mara mbili ndipo alipomshinda. Akaishi na mkewe akajifungua. Hata hivyo ilibainika kuwa mtoto yule hakuwa wa kwake ila wa jini. Na akamtokea na kumwambia ampeleke porini na kuelekezwa sehemu, akampeleka. Jini anamwambia hana shida na yeye kumdhuru, aendelee na tu mkewe kwani shida yake ilikuwa ni kuzaa na binadamu. Mkewe na rafiki zake walikuwa wanamtafuta, wakamkuta porini. Baada ya hapo jini hakuonekana tena, furaha ikarejea kwenye ndoa.



# Harmonize aibua makubwa

MWANAMUZIKI na mmiliki wa lebo ya Konde Gang Music, Harmonize, amechafua hali ya hewa baada ya kauli yake ya kuunga mkono 'maDJ's' wa Kitanzania kutopiga miziki ya Kitanzania.

Kwa mujibu wa Harmonize, nyimbo za kibongo nyingi haziwezi kupigwa katika kumbi za starehe kutokana na ujumbe wao kujaa maneno yanayogusa viungo nyeti ambavyo vinaweka ukakasi kusikiliza.

Akizungumza na mashabiki zake kupitia 'Insta Story', Harmonzie amesema nyimbo hizo badala ya kujenga na kukuza lugha ya Kiswahili, zimekuwa na ladha mbaya na inawaletea shida maDJ kuzicheza.

"Napenda jinsi ma-DJ's wa Tanzania kutocheza sana muziki wa Bongo Club, tunataja sana viungo vya pilau kwenye ngoma zetu, tunatakiwa kubadilika, tunawapa shida waache kupiga nyimbo kama mazerati, no stress, woman au mapiano sound halafu wakapige pembe la ng'ombe ukiuliza ni uzalendo, hivyo tutakuwa hatutangazi bali tunaua lugha yetu nzuri ya Kiswahili kwa sauti mbaya tunazozitumia," ameeleza Harmonize.





# 'Tumewamisi' kwenye hip hop

**Na Adam Fungamwango**

MUZIKI wa kufokafoka maarufu kama 'hip hop' ni kama umeanza kufifia kwenye gemu la muziki bongo, ingawa kuna wasanii kadhaa wanakomaa ili kuendelea kuwapo.

Muziki wa bongo fleva ambao staili yake ni kuimba zaidi kuliko 'kuchana' ndiyo ulioonekana kuumeza muziki huo kwa sasa.

Wasanii kama Roma Mkatoliki, Stamina, Nay wa Mitego na Dogo Janja, ndiyo angalau wanaufanya uendelee kuishi, huku rapa mwenzao Mwana FA, akiwa tayari ameshaingia kwenye majukumu mengine ya kisiasa kwa kuchaguliwa kuwa Mbunge wa Jimbo la Muheza sasa anajulikana kama Mh. Hamisi Mwinjuma.

Leo tunawakumbuka wasanii wa muziki huo waliotamba kuanzia miaka ya 2000 na kuufanya muziki huo kufanya vema kwenye soko la muziki Tanzania.

**1. JOSEPH MBILINYI 'MR 2 SUGU'**

Ni mmoja kati ya waasisi na muziki huu wa kufokafoka, tangu wakati baadhi ya watu hawauelewi vizuri na kuonekana kama wa watu wakorofi, wahuni.

Yeye na Joseph Haule maarufu kama 'Profesa Jay', na wengine wachache, walikomaa na kubadilisha aina ya maudhui ya nyimbo na kuimba vitu ambavyo vilianza kuwakuna hata watu wazima na kuanza kuukubali muziki huo, ulikuwa ukiangazia matatizo ya kijamii zaidi, badala ya mapenzi.

Nyimbo kama 'Wananita Sugu' na 'Sugu Moto Chini' zilimtangaza na kumfanya ajizolee mashabiki wengi.

Kwa sasa si Mbunge wa Jimbo la Mbeya Mjini, hivyo inawezekana akawa na nafasi ya kujerea tena kwenye 'gemu' na kuurudisha tena muziki huo juu.

**2. PROFESA JAY**

Kwa hakika huyu ndiye aliyebadilisha aina ya 'meseji' kwenye muziki wa 'hip hop' ambapo awali zilionekana kama ni za kihuni, lakini alizungumzia maisha ya kila siku kwenye jamii, kwa kiwango kilichowafanya hata watu wazima kuanza kuukubali muziki huo.

Ngoma kama 'Ndiyo Mzee', 'Bongo Dar es Salaam', 'Zali la Mentali' zilimfanya kuwa maarufu.

Akawa Mbunge wa Jimbo la Mikumi. Kwa sasa si mbunge tena. Afadhali Jay alikuwa akitoa mara moja moja ngoma huku akiwa mbunge. Je, atarejea kuisimamisha tena 'hip hop?'

**3. INSPEKTA HAROUN**

Aliufanya muziki wa hip hop kupendwa hata na kinadada kutokana na aina yake ya utunzi.

Marapa wengi kupenda zaidi kuimba nyimbo ngumu, za kijamii, kisiasa na uchumi, lakini Inspekta Haroun alifanya mabadiliko kidogo na kutunga nyimbo za mapenzi kwa mtindo huo wa hip hop.

Nyimbo kama 'Asali wa Moyo' na 'Mtoto wa Geti Kali' ziliondokea kupendwa na kumfanya kuwa mmoja wa wasanii maarufu sana mwanzoni mwa miaka ya 2000. Kwa sasa amekuwa hasikiki sana. Hata kama yupo kwenye gemu, lakini si kama zamani, huku mwenzake Nature akiwa anajikongoja.

**4. JAY MOE**

Huyu ni mmoja wa marapa aliyeleta vitu tofauti kwenye staili ya muziki huo. Jina halisi ni Juma Mchopanga.

Kuna aina fulani ya vionjo aliviingiza kwenye muziki huo na kuufanya uvutie zaidi, hasa kwenye mapigo tofauti na kina Sugu na Profesa Jay ambao ulionekana ni wa kusikiliza 'meseji' zaidi.

Alijizoelea mashabiki wengi pia kutokana na kutoa vibao vilivyovuma kama moto wa nyika kama 'Bishoo', 'Jua na Mvua' na, 'Kama Unataka Demu'.

Ingawa hivi kwenye miaka ya karibuni amekuwa akitoa ngoma. Lakini bado si kama Jay Moe yule wa miaka ya 2000.

**5. AFANDE SELE**

Alitawazwa kuwa mfalme wa Rhymes, aliposhinda kwenye shindano hilo mwaka 2004 jijini Dar es Salaam, akiwashinda wasanii wengi maarufu wa muziki huo waliokuwapo wakati huo.

Ni rapa mkongwe nchini, ni mmoja wa wasanii waliochangia kuufikisha muziki wa hip hop hapa ulipo. Nyimbo zilizompa umaarufu mkubwa ni 'Darubini Kali', 'Mtazamo', 'Ndugu' zangu na nyingine nyingi.

Naye alijiingiza kwenye masuala ya siasa, na shughuli zingine.

Kama anaendelea na muziki, si kama ilivyokuwa zamani.



# Mke wa Peter Okoye atamani P square

MKE wa mwanamuziki nyota wa Nigeria, Peter Okoye, ameamua kuvunja ukimya baada ya kumtaka mume wake na pacha mwenzake, Paul Okoye, kutambua wao ni ndugu na kamwe hawawezi kutengana.

Mwanamke hiyo, OLola Omotayo, akitumia ukurasa wake wa Istagram, aliwashauri Paul na Peter, kuwa wapende wasipende wao watabaki kuwa mapacha na ndugu wa damu na siku ya kuzaliwa itabaki kuwa ni moja.

"Hmmm....kwa mapacha mpende msipende nyinyi ni ndugu, na si hivyo tu, nyinyi ni mapacha, nawatakia siku njema ya kuzaliwa kwenu," ameandika Lola.



## Rahama mwana kulitafuta, mwana kulipata

POLISI nchini Nigeria wanamchunguza mwigizaji kutoka Kannywood, Rahama Sadau, baada ya picha zake zilizomuacha wazi nusu ya mwili wake kuzua utata.

Taarifa kutoka ofisi ya Inspekta Jenerali wa Polisi (IGP), Mohammed Adam, amesema amemwagiza Kamishna wa Polisi wa Jimbo la Kaduna, Umar Muri, amchunguze mwigizaji huyo.

Kulingana na Ofisa Mkuu wa Wafanyakazi ofisi ya IGP, Idowu Owohunwa, kamishna huyo ametakiwa aangalie suala hilo ambalo limezua malalamiko yaliyopelekea kuibuka kwa kashfa.

## Uchemba ndoa imekunogesha

MSANII wa filamu kutoka Nollywood, Williams Uchemba, hatimaye amefunga ndoa na mpenzi wake wa siku nyingi.

Harusi hiyo iliyofanyika mwishoni mwa wiki iliyopita, ilifanyika kwa kuzingatia sherehe za kitamaduni.

Katika harusi hiyo mastaa mbalimbali walihudhuria wakiwamo waigizaji, wanamuziki, rafiki wa karibu na ndugu na jamaa wa msanii huyo.





## Olivia, Jason wabwagana

STAA wa filamu wa Marekani, Olivia Wilde na mpenzi wake, Jason Sudeikis, wameachana baada ya kuishi kama wachumba kwa miaka kumi.

"Tumeamua kwa njia ya amani, tumekuwa katika utaratibu kama wazazi wazuri na watoto wetu ndio kipaumbele na moyo wa uhusiano wa kifamilia,"

Wilde na Sudeikis wana watoto wawili, wa kiume, Otis Alexander (6) na msichana, Daisy Josephine (4).

## Duuh! Frederick miaka 44 bila mke?

MWIGIZAJI mkongwe kutoka Nollywood, Frederick Leonard, ameamua kuzungumzia maisha yake ikiwamo kukaa singo wakati ametimiza miaka 44.

Amesema kuwa na umri huo halazimiki kuwa na mke, ingawa vitabu vya dini vinamtaka kila mwanamume kuwa na mwenza wake wa halali.

"Sijapoteza matumaini ya kuoa, ni muda tu haujafika, ninaamini ni jambo la heri ambalo Biblia imesema si vizuri kwa mwanamume kukaa bila kuoa. Lakini Sitaki kufika mwisho nikiwa peke yangu," amesema.



# MTAFUTANO TIGRAY

- Dk. Tedros Ghebreyesus ahusishwa
- Kamatakamata yaongeza wasiwasi

**Na Moshi Lusonzo**

MGOGORO kati ya serikali ya Ethiopia na waasi wa jimbo la Tigray, unazidi kutanuka na sasa baadhi ya wanasiasa wa ngazi za juu wanahusishwa kufadhili vita.

Mvutano kati ya serikali ya Shirikisho inayoongozwa na Waziri Mkuu, Abiy Ahmed na uongozi wa jimbo hilo lililopo kaskazini mwa nchi hiyo, ulianza kidogokidogo, lakini sasa hali imekuwa ya kutisha baada ya majeshi kila upande kukabiliana kwa silaha.

Katika hali ya kushangaza, wiki hii mgogoro huo umepata sura mpya baada ya Mkuu wa majeshi ya Ethiopia, kumnyooshea kidole Mkurugenzi wa Shirika la Afya Duniani (WHO) Dk. Tedros Adhanom Ghebreyesus, kufanya ushawishi kwa maslahi ya chama cha Tigray People's Liberation Front (TPLF), kinachopambana na majeshi ya serikali.

Mapaka sasa mamia ya raia wameuawa katika mapambano yanayoendelea ndani ya Tigray, tangu mwanzoni mwa mwezi Novemba.

Dk. Ghebreyesus anatoka katika jamii ya Watigray na alikuwa waziri wa afya katika serikali iliyopita ya Ethiopia, iliyoongozwa na TPLF.

Hata hivyo, kiongozi huyo hajajibu tuhuma hizo.

Mkuu huyo wa majeshi, Jenerali Berhanu Jula, amewaambia wanahabari kuwa Dk. Ghebreyesus, anafanya kampeni za chini kwa chini kuwasaidia waasi hao kupata silaha.

"Anafanya kila awezalo kuunga mkono chama cha TPLF na kuwasaidia kupata silaha," amesema bila kutoa ushahidi.

Ameongeza "Hatumtarajii kuunga mkono Waethiopia na kukemea watu hawa. Amekuwa akifanya kila kitu kuwaunga mkono, amefanya kampeni ili nchi jirani zikemee vita. Amewafanyia kazi ili wapate silaha."

Ghebreyesus, alichaguliwa kuongoza WHO mwaka 2017, na jina lake lilijitokeza na kuwa maarufu baada ya kuibuka kwa janga la virusi vya corona.



Mkurugenzi mkuu wa WHO, Dk. Tedros Ghebreyesus. . **PICHA: MTANDAO.**

**DK. GHEBREYESUS NI NANI?**

DK. Tedros Ghebreyesus, alizaliwa katika mji wa Asmara, ambao wakati huo ilikuwa nchini ya Ethiopia, kabla ya Eritrea kujitenga na kuufanya mji wake mkuu.

Baba yake Adhanom Gebreyesus na mama Melashu Weldegabir, walitoka katika eneo la Enderta awrajja katika jimbo la Tigray.

Dk. Ghebreyesus, anakumbuka mambo mengu magumu aliyopitia wakati akiwa mtoto ikiwamo kumshuhudia mdogo wake akifariki baada ya kuugua ugonjwa wa malaria.

Mnamo mwaka 1986, alipokea Shahada yake ya kwanza Sayansi kutoka Chuo Kikuu cha Asmara. Pia alisoma chuo cha London School of Hygiene & Tropical Medicine cha Uingereza na kupewa shahada ya uzamili ya Sayansi katika eneo la kinga ya magonjwa ya kuambukiza mwaka 1992.

Mwaka 2000, alipata shahada ya uzamivu ya Udaktari wa Falsafa katika afya ya jamii kutoka Chuo Kikuu cha Nottingham cha Uingereza.

**NI MWISHO WA TPLF?**

Mapigano yanayoendelea katika jimbo hilo, pengine itakuwa mwisho wa chama cha (TPLF) baada ya wanachama wake wengi kukamatwa au kukimbilia uhamishoni.

Waziri Mkuu Abiy, hivi karibuni amesema majeshi yanapata ushindi na wanakaribia mji wa Mekelle, ambao ni makao makuu ya Tigray.

Tayari jeshi la polisi kutoka shirikisho limetoa hati ya kukamatwa kwa maofisa 76 wa kijeshi, baadhi yao wanadaiwa kuwa ni wastaafu ambao wanatuhumiwa kushirikiana na TPLF.

Akizungumza na BBC, Billene Seyoum, msemaji wa Waziri Mkuu, amepinga madai kwamba Watigray wanaoishi maeneo mengine wanakamatwa kwa misingi ya kikabila.

Mgogoro huo umeanza muda mrefu kati (TPLF) na serikali kuu ya Ethiopia.

Mambo yalizidi kuwa mabaya baada ya Waziri Mkuu wa Ethiopia, Abiy Ahmed, kuahirisha uchaguzi kutokana na janga la corona, lakini TPLF ilichukulia hatua hiyo ya serikali kuu ni batili ikadai kuwa kiongozi huyo hana mamlaka ya kuendelea kuongoza nchi.

Baadae serikali inailaumu TPLF kwa kushambulia kambi ya kijeshi kwa lengo la kuiba silaha, madai ambayo chama hicho iliyakana.

Kiongozi wa TPLF, Debretsion Gebremichael, ambaye ni mzaliwa wa Shire, amethibitisha katika televisheni moja jimboni humo kwamba wanajeshi wake wamepoteza udhibiti wa miji ya Kusini na Magharibi mwa Tigray.

**MAJIRANI WAZIDIWA**

Nchi jirani zimeanza kutoa wito wa suluhu baada ya kuelemewa na wakimbizi ambao wamekimbilia katika nchi hizo kunusuru maisha yao.

Sudan inasema watu 36,000 wameingia nchini humo kupitia mpaka wa Tigray, wakati mapigano yakiendelea.

Hata hivyo, Umoja wa Mataifa umeonya kutokea kwa mzozo kamili wa kibinadamu.

"Huenda kukawa na watu wengi waliokimbia makazi yao ndani ya Tigray, hali ambayo inastahili kuangaliwa wakati tunapojiandaa kuwasaidia kadili ya uwezo wetu," anasema Jens Lark, msemaji wa ofisi ya umoja huo inayeshughulikia masuala ya kibinadamu (OCHA).

**MAMBO MUHIMU KUHUSU TIGRAY**

Jimbo hilo ndiko kulikuwa na Ufalme wa Aksum, ikielezwa ni sehemu yenye alama ya ustaarabu wa ulimwengu wa zamani.

Kuna wakati eneo hilo lilikuwa na utawala wenye kuvu zaidi kati ya milki za Kirumi na Uajemi.

Magofu yaliyoko ndani ya miji wa Aksum yametambuliwa na Umoja wa Mataifa kama eneo la turathi za kale duniani. Eneo hilo ambalo limekuwepo kati ya karne ya kwanza hadi ya tatu AD, linajumuisha , makasri, makaburi ya wafalme na kanisa linaloaminiwa na baadhi ya watu kuwa sanduku la agano la kale.

Watu wengi katika eneo la Tigray ni Wakristo wa dhehebu la Orthodox Ethiopia. Mzizi wa Dini ya Kikristo ulianza miaka 1,600 iliyopita.

4. Lugha kuu katika eneo hilo ni Tigrinya, lahaja ya Kisemeti ina wasemaji wasiopungua milioni saba ulimwenguni.

5. Ufuta ni zao kuu la biashara, unasafirishwa Marekani, China na nchi nyingine



Moshi wa mabomu ukitawala eneo moja la Tigray

MAKALA

# Waziri Elimu ajaye aanze na:

## Kuwezesha walioelimika kujiajiri
## Vyuo vikuu kuwa vituo vya weledi

NA GAUDENSIA MNGUMI

MOJA ya maeneo muhimu kufanyiwa kazi wakati wa muhula wa pili wa awamu ya tano ni kuondoa changamoto iliyopo leo kwa taasisi hasa vyuo vikuu na vya kati kufunza wasomi ili waweze kujitegemea na kulitegemeza taifa.

Ni kwa sababu inavyoonekana vinazalisha wahitumu tegemezi pengine wasio na hatma ili kumudu maisha yao.

Jukumu la Waziri wa Elimu ajaye ni kukabiliana na uwezo mdogo wa wanafunzi wa vyuo vikuu ambao licha ya kuelimika wanashindwa kujianzishia ajira zenye tija kumudu maisha yao , badala yake wanategemea kuajiriwa.

Baadhi wakizungukia maofisini kila leo kuulizia ajira wakiwa wamebeba vyeti kwenye bahasha za khaki ambazo zimechanika na kuchakaa ikiashiria kukata tamaa.

Wakati hayo yakitokea vyuo vikuu vinatamba kuwa vinaandaa wasomi wanaoweza kujiajiri, vikitamba na kutaja mipango na mikakati iliyopo lakini ukweli ni kwamba havijaweza kutimiza azma hiyo.

Waziri wa Elimu mtarajiwa na wataalamu wa masuala ya kazi wanachotakiwa sasa ni kufanyakazi na kuwezesha mipango na mikakati ya kuandaa wasomi kujiajiri na kuifanya hali hiyo iakisi ukweli kuwa Tanzania ni nchi ya uchumi wa kati kwa matendo.

Licha ya kuwapo maelezo kuwa vyuo vikuu vinawafundisha wanafunzi hao kukabiliana na matatizo ya ukosefu wa ajira, hakujawa na jitihada za kutosha kufanikisha azma hiyo, hivyo Waziri wa Elimu ajaye, akumbuke hilo.

**MIKAKATI MADHUBUTI**

Pengine kukosekana mikakati ya wanafunzi kujianzishia ajira binafsi, pia uhaba wa kazi na taasisi za elimu ya juu kushindwa kutatua tatizo hilo ni 'jipu' linalovimba na kuongeza maumivu kila siku.

Kwa hiyo ni wakati wa kuwa na mipango na mikakati ya kubadili sera na taratibu za kufundisha ili kuwaandalia wahitimu hatma na kuondokana na wimbi la kuzurura kusaka kazi kila uchao.

Ni nini kifanyike sasa? Ndilo swali la kila mmoja, hivyo wasomi, watunga sera, wataalamu wa ajira walijibu kwa kuanza na kupunguza kubadilisha utaratibu wa kufundisha ili uangalie jinsi ya kuwaandaa vijana kumudu maisha yao badala ya kuangalia alama za kufaulu kama A na B au 'sifuri.'

Utaratibu uende mbali kwa kuchambua uwezo wa mwanafunzi kuchangia maendeleo yake ya taifa kwa kuwafundisha ujasiriamali na kujitegemea kunakotokana na rasilimali zinazopatikana kupitia kozi wanazozisoma madarasani.

Iwapo mtazamo huo ukibadilika pengine utawezesha kuviingiza vipaumbele vya maendeleo kwenye taaluma ambapo wanafunzi watafunzwa jinsi ya kutumia elimu walizopata kujiendeleza na kutatua matatizo ya jamii zao.

Pia rasilimali nyingi zilizoko nchini zitumike kupunguza tatizo la ajira kwa mfano kwenye migodi ya vito na dhahabu, mistu, wanyamapori , ardhi na maji.

Pia vyuo vikuu na vya kati viwe mfano wa maeneo ya kuelimisha na kufunza vijana kujiajiri mfano Chuo Kikuu cha Kilimo cha Sokoine (SUA) kinachotoa mafunzo ya kilimo na ufugaji, sayansi na teknolojia vitafsiri elimu inayotolewa kwa matendo ili ibadilishe maisha ya wahitimu wake, majirani wanaowazunguka chuo na hata Mkoa wa Morogoro.

SUA inaweza kulenga kwenye kuwa na mashamba darasa na kituo cha umahiri wa masuala yanayoendana na kilimo, uvuvi, ufugaji, uundaji wa zana za kilimo na teknolojia za kilimo.



Mkuu wa Chuo Kikuu cha Dar es Salaam na Rais Mstaafu, Dkt.Jakaya Mrisho Kikwete, akisalimiana na Mwenyekiti wa Baraza la Chuo Kikuu cha Dar es Salaam, Jaji Damian Lubuva, kabla ya kuwatunuku wahitimu vyeti vya shahada na stashahada.. **PICHA MTANDAO.**

Ni wakati wa vyuo kuonyesha kwa vitendo na umahiri elimu inayotolewa inavyobadili maisha na kutengeneza ajira. Ndiyo masuala ya shamba darasa liwe la mazao, teknolojia, ufugaji, kuchimba madini, uzalishaji viwandani na miradi inayotumia matokeo ya utafiti unaofanywa na vyuo ili watu na wanafunzi kujifunza.

Vyuo kama Chuo Kikuu cha Ushirika Moshi (MOCU) kinaweza kuwa mfano na kioo cha kuitazama jamii na kuibadilisha kiuwekezaji kwa kuiwezesha kuigiza mifano ya miradi ya uwekezaji, ujasiriamali ubunifu wa biashara kwa kuona mifano inayosimamiwa na chuo hicho ili wanafunzi na jamii ijifunze.

**KUJIFUNZA UKWELI**

Awamu ya lala salama ya muhula wa pili wa awamu ya tano, ni wakati wa kuhakikisha kuwa ufundishaji unatoka nje ya vitabu, elimu za kinadharia, kukariri na mihadhara ambayo haiakisi uhalisia wa mambo.

Lakini pia kujali alama za kufaulu kwa kuangalia A, B+ mambo hayo yawekwe kando, ufundishaji uende mbele kutafsiri elimu zinazotolewa kwa kuzihusisha na rasilimali zilizopo na kuwafundisha wanafunzi ubunifu wa kuchanganya taaluma na mazingira yanayozunguka na rasilimali zilizopo ili waanzishe miradi na kumudu maisha yao.

Elimu ya juu isaidie wanafunzi kuona jinsi watakavyoweza kujiajiri wakitumia rasilimali kwa mfano bahari, ardhi, madini, mifugo, mazao kama viungo, maua na vivutia watalii kutengeneza kazi nyingi hata kuanzisha viwanda ili kubadili maisha yao.

**KUSHIRIKISHA WADAU/UTAFITI**

Si kila kinachosemwa na serikali kuhusu elimu ya juu kiko sahihi. Wakuu wa vyuo, serikali na wadau wengine wa taaluma, wajiri, masuala ya kazi na watafiti washirikiane kuibua upungufu uliko vyuoni.

Vigogo wa vyuo waelezwe wanapokosea, iwe ni kwenye kuandaa wasomi wa elimu ya juu ili waweze kuwapika wajitegemee na kutumikia taifa kwa kuajiri na kujiajiri.

Vyuo vya kati na vikuu vinahitaji maoni ya wadau kwenye kutatua tatizo la ajira na kuinua elimu hivyo kila mwaka wawe wakiandaa kongamano la wadau kupeana mikakati ya kuboresha taasisi za elimu hasa vyuo vya kati na vya elimu ya juu.

Serikali, vyuo na vyuo vikuu katika mazingira ya leo ya kusaka kazi ni kwamba havizalishi ajira vinapika wasomi na wataalamu ambao watachukuliwa na wanaotengeneza kazi ambao ni `waajiri' hivyo, wanapokutana wanapata fursa kueleza wanachofanya ili taasisi za elimu zijifunze.

Sekta binafsi na wawekezaji wanaeleza aina ya kazi walizonazo, mambo wanayotaka yazingatiwe kuboresha mahitaji yao kwenye kufundisha vyuoni, serikali inataja mipango yake, wanafunzi na kila mmoja anabainisha atakavyosaidia mchakato akitaja fursa na ushauri utakaozingatiwa.

Ni mambo yanayotakiwa kufanyika kila mwaka ili kupunguza makali ya kukosekana ajira rasmi lakini pia wanafunzi kushindwa kujiajili na kuandaa mikakati ya ubunifu ya kuwawezesha zaidi kwenye elimu ya juu yenye manufaa.

**UWEKEZAJI ELIMU**

Mafanikio ya uchumi yanayoleta maendeleo yanaanzia kwenye elimu ya juu hivyo, kufanikiwa elimu hiyo kutaboresha elimu ya msingi, afya, kilimo, siasa hivyo awamu ya tano iwekeze zaidi.

# Kasri la Nabii lashikiliwa

**PRETORIA,** Afrika Kusini

MALI za nabii bilionea kutoka Malawi, Shepherd Bushiri na mkewe Mary, zimekamatwa na kushikiliwa na serikali ya Afrika Kusini, baada ya kutoroka kutokana na kukabiliwa na kesi ya utakatishaji wa fedha.

Moja ya mali inayoshikiliwa ni kasri la kifahari ililopo karibu na mji wa Pretoria, lenye thamani ya randi milioni 5.5, sawa na Sh. milioni 810.

Kulingana na taarifa zilizopatikana jana, Jaji wa mahakama moja nchini humo aliwaamuru Nabii Bushiri na mke wake kutoa stakabadhi za nyumba hiyo wakati walipopewa dhamana kufuatia kesi 419 walizofunguliwa wakituhumiwa kwa utakatishaji wa fedha na ufisadi.

Wakati huo huo, wahubiri hao jana waliachiliwa huru baada ya kukamatwa na kufikishwa mahakamani nchini Malawi.

Nabii Bushiri na mke wake, walikana kuhusika na tuhuma hizo kupitia ujumbe waliotuma kwenye mitandao ya kijamii wakidai walirudi Malawi kwa kuhofia usalama wao.

Tayari Afrika Kusini, ilishatoa kibali cha kuwakamata wawili hao na waliomba serikali ya Malawi ziwarejeshe nchini humo kukabiliana na kesi yao.

Nabii Bushiri ambaye ni mzaliwa wa Malawi, anaendesha shughuli zake za kidini katika makanisa mbalimbali ikiwamo Ghana na Afrika Kusini.

Katika mambo mbalimbali ambayo kiongozi huyo wa kidini anadai anaweza kutibu ni ugonjwa wa Ukimwi, kulingana na magazeti ya Afrika Kusini ya Mail & Guardian yaliyotolewa mwaka 2018.

Bushiri alimtabiria mwanasiasa wa Zimbabwe Kembo Mohadi, kuwa atapata madaraka ya juu, kabla ya kutangazwa kuwa makamu wa rais wa nchi hiyo.

Nabii Bushiri anafahamika kama ndiye kiongozi wa kidini tajiri zaidi barani Afrika.

Botswana imempiga marufuku kukanyaga katika ardhi ya nchi hiyo kwasababu ya kuhusishwa na pesa za miujiza.

Hata hivyo, kiongozi hiyo amekuwa maarufu kutokana na kukusanya idadi kubwa wafuasi wake katika viwanja vikubwa vya michezo.

BBC



Bushiri na mkewe Mary, ambao walikamatwa siku ya Jumatano kutokana na ombi la Afrika Kusini kurudishwa nchini humo kukabiliana na kesi zao **(Picha: RF). PICHA: OMPR – ZNZ.**

# Wanamgambo Tigray washambulia Amhara

**ADIS ABABA,** Ethiopia

WANAMGAMBO wa jimbo la Tigray, wamefyatua makombora mengine kuulenga mji wa Bahir Dar ulioko jimbo jirani la Amhara.

Hata hivyo, makombora hayo hayajasababisha madhara kwa binadamu wala kuharibu mali.

Kwa mujibu wa taarifa kutoka serikali ya Amhara, urushaji wa makombora hayo yalifanyika wakati vikosi vya serikali ya shirikisho vikielekea mji mkuu wa jimbo la Tigray, Mekelle.

Ofisi ya mawasiliano ya serikali ya Amhara, ilisema kundi la Ukombozi wa Watu wa Tigray (TPLF) lilifyatua makombora hayo usiku wa manane kuamkia jana.

Jimbo hilo ambalo lina mgogoro wa muda mrefu wa mpaka na Tigray, liliwatuma wanajeshi wake kuviunga mkono vikosi vya serikali ya shirikisho.

Wakati huo huo, Mkuu wa Shirika la Afya duniani (WHO), Tedros Ghebreyesus, amekanusha madai yaliyotolewa na mkuu wa jeshi la Ethiopia, kuwa anasaidia waasi kuwapatia silaha na msaada mwingine.

Ghebreyesus ambaye ni raia wa Ethiopia alisema madai hayo hayana ukweli na kwamba yeye binafsi anaunga mkono upatikanaji wa amani na kutoa wito kwa kila upande kupunguza mvutano kwenye mzozo huo.

DW

## Kanisa kuchunguza Istagram ya Papa

**ROME,** Vatcan

KANISA la Katoliki linachunguza akaunti ya Instagram ya Papa Francis, baada ya kuibuka kwa mjadala kutokana na kuweka alama ya kuipenda picha ya mlimbwende wa Brazil, ambaye alikuwa hajavaa nguo yenye staha.

Hata hivyo, taarifa kutoka makao makuu Vatcan, haijaweka wazi ni lini tukio hilo lilifanyika dhidi ya mwanamke huyo, Natalia Garibotto, ambaye alikuwa amevaa sare ya shule.

Vyombo vya habari vilianza kuripoti kuhusu taarifa hiyo Ijumaa iliyopita , kabla ya kuondolewa kwa alama hiyo haraka.

Maofisa wa baba mtakatifu wameripotiwa kufanya uchunguzi kujua namna akaunti hiyo ilivyopelekea kuipenda picha hiyo.

"Hatuwezi kusema kuwa ni Baba Mtakatifu ndio aliyebonyeza kitufe cha kupenda picha ile, na inabidi tupate ufafanuzi kutoka Instagram ,"alisema msemaji wa Vatican.

Akaunti ya Instagram ya Papa ambayo ina jina la franciscus, ina wafuasi milioni 7.4 kutoka duniani kote.

Vyanzo vya karibu na Vatican, vilisema akaunti hiyo inaongozwa na kikosi cha wafanyakazi na uchunguzi wa ndani unaendelea.

BBC

## Waliokufa Uganda wafikia 30

**AMPALA,** Uganda

IDADI ya waliopoteza maisha kufuatia vurugu zilizotokea katika kampeni nchini Uganda, imefikia watu 30 mpaka jana.

Akizungumzia machafuko hayo kwa mara ya kwanza, Rais Yoweri Museveni, alionya wale waliohusika katika kuchochea ghasia hizo watakiona cha mtema kuni na analaumu nchi za kigeni kufadhili machafuko hayo.

Hata hivyo, wanaharakati wa haki za binadamu waliikosoa tume ya uchaguzi ya nchi hiyo kwa kushindwa kudhibiti vyombo vya usalama ambavyo vinadaiwa kusababisha mauaji hayo kwa watu wasio na hatia.

Taarifa ya polisi ilisema licha ya idadi ya watu hao waliokufa, wengine zaidi ya sitini wapo katika hali ya mahututi baada ya kujeruhiwa vibaya.

Miongoni mwao majeruhi ni waandishi wa habari watatu. Kulingana na taarifa hiyo, watu 48 wana majeraha ya risasi.

Mgombea urais kutoka chama cha upinzani, Robert Kyagulanyi, maarufu kama Bobi Wine, alitarajiwa kufikishwa mahakamani mjini Iganga, kilomita 110 kutoka Kampala.

Kyagulanyi alikamatwa siku ya Jumatatu kwa madai ya kukiuka kanuni za kudhibiti ugonjwa wa COVID-19 baada ya kuwakusanya watu zaidi ya mia mbili.

DW

# MATANGAZO MCHANGANYIKO

## VIWANJA/MASHAMBA

**PATA MKOPO WA HARAKA KWA MASHARTI NAFUU KUTOKA EFL**
Mkopo umelenga dharura na mahitaji mengine kama vile:

- **Kuboresha biashara**
- **Kulipa kodi ya nyumba**
- **Kumalizia tenda**
- **Kulipa matibabu n.k.**

Mawasiliano yetu:
**Dar es salaam – 0768 928 516.**
**Arusha – 0677 226 960.**

## NAFASI ZA MASOMO

**KELAND NURSERY AND PRIMARY SCHOOL** ILIYOPO SALASALA RTD INATANGAZA NAFASI ZA AWALI NA MSINGI. KWA MAWASILIANO **PIGA SIMU: 0713 327613.**

## NYUMBA/MASHAMBA

**NYUMBA INAUZWA,** Nyumba inauzwa ni ya ghorofa moja, ina frem tatu za biashara zote zina wapangaji. Bei maelewano, ipo Ukonga Dar es salaam. Piga simu namba **0757 079 057.**

NIPASHE NI JIBU LAKO
NJOO UTANGAZE NASI
KWA BEI NAFUU SANA
Tutumie E-mail: advertise@guardian.co.tz, au piga simu: 0782253676

## KUPOTEA KWA VYETI



**GOODLUCK JACKSON** anatangaza kupotelewa kwa vyeti,cha kidato cha nne index namba **S.1163/0256** kilichotolewa na shule ya secondary UJENZI mwaka 2014,cheti cha ya kidato cha nne cha kurisiti index namba **P.1619/0047** shule ya secondary VICTORY mwaka 2017 na result slip ya kidato cha sita yenye index namba **S.1071/0619** iliyotolewa na shule ya secondary **ST.MATTHEW'S** mwaka 2020, yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi. Polisi taarifa **DAR/MBA/RB/806790/2020**

116007802

## KUPOTEA KWA RESULT SLIP



**RAYMOND DOMINIC KISHIWA** anatangaza kupotelewa kwa result slip na leaving certificate ya kidato cha sita vyenye **index namba S 0386/0555** vilivyotolewa na baraza la mtihani kupitia shule ya secondary ya GEITA mwaka 2020,yeyote atakayeviokota atoe taarifa kituo chochote cha polisi Polisi taarifa **GE/TR/RB/6504/2020**

116008202

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA WILAYA MOROGORO**
**MAOMBI NA. 40 YA MWAKA 2020.**

**ABDULATIF T.MOHAMED**
**ABDULATIF TAALIB MOHAMED**
**ATN PETROLEUM COMPANY LIMITED**
**AT AND T.TRANSPORT COMPANY....................MLETA MAOMBI**

**DHIDI YA**

**ISACK KATAMITI**
**CLINTON JOHN HOSTEN**
**HASHIM FARHAN FAYA**
**JOSEPH ALEX CHIKOTO**
**DEBORA JOHN NKYA.......................................WAJIBU MAOMBI**

**WITO/KUITWA SHAURINI KWA**
**CLINTON JOHN HOSTEN**
**JOSEPH ALEX CHIKOTO**

Popote walipo mnaarifiwa mfike katika baraza la ardhi na Nyumba la wilaya ya Morogoro tarehe 10/12/2020 nyie wenyewe binafsi au wawakilishi wenu bila kukosa ambapo maombi yamepangwa kutajwa.Endapo hamtaudhuria maombi yatatajwa na kusikilizwa upande mmoja dhidi yenu na kutolewa uamuzi.

**Imetolewa kwa mkono wangu leo tarehe 18 Mwezi November,2020.**

MWENYEKITI
BARAZA LA ARDHI NA NYUMBA (W)
MOROGORO

116008402

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO MJINI**
**USIMAMIZI WA MIRATHI FORM II**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA YA 5 KANUNI YA 2)**
**Katika mahakama ya mwanzo CHAMWINO MJINI**
**Usimamizi wa mirathi 107 2020**

**Ombi la ABSOLOMON MWANKUSYE kuteuliwa kuwa Msimamizi wa mirathi ya Marehemu DAVID ABSOLOMON MWANKUSYE**

**KWA YEYOTE ANAYEHUSIKA NA MIRATHI HII TANZANIA BARA.**

Watu wote wanaodaiwa kuwa na uhusiano wowote na Mirathi ya Marehemu huyo wanaalikwa kuja, kuhudhuria kesi wakitaka mnamo tarehe 24/11/2020 huyo mwombaji kabla hajateuliwa kuwa msimamizi wa Mirathi hiyo.
Wosia Wa Marehemu huyo upo Mahakamani waweza kukaguliwa. Tarehe 20/11/2020

Tarehe 20/11/2020
SAHIHI YA HAKIMU
HAKIMU MAHAKAMA YA MWANZO CHAMWINO-MJINI DODOMA

116009002

## KUPOTELEWA NA KADI YA GARI

**FRANK CONSTANTINE MUSHI** anatangaza kupotelewa na kadi yake ya gari yenye namba za usajili **T 179 BDW – TREKTA MASSEY FERGUSON. CHASSIS NO-650983.** Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/CEN/RB/740112/2020.**

216008902

## KUPOTEA KWA CHETI



**STEPHANO ROBERT CHILEWA** anatangaza kupotea kwa cheti cha kidato cha nne chenye index namba **S.5105/0031** kilichotolewa na Baraza la Mitihani kupitia **UMAWANJO BOYS SEKONDARI** mwaka 2017. Yeyote atakayeiona atoe taarifa kituo cha polisi. Taarifa ya Polisi: **DAR/MAG/RB/812753/2020.**

116009102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;345/2020**
**Ombi la DEUDATUS P.MKAMATI,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu JANETH DEO MKAMATI.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 01/12/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 16/11/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU

116008102

**JAMHURI YA MUUNGANO WA TANZANIA**
**MAHAKAMA USIMAMIZI WA MIRATHI**
**(S.M.M.1984 NYONGEZA) YA 5 KANUNI YA 2**
**Katika mahakama ya mwanzo MJINI-MOROGORO**
**Usimamizi wa mirathi No;353/2020**
**Ombi la FADILA TWAHA MHANDO,Kuteuliwa msimamizi wa mirathi marehemu TWAHA SHABANI MHANDO.**

Watu wote wanaodai kuwa na uhusiano wowote na mirathi ya marehemu kuwa wanaarikwa kuja na kuudhuria shaurini mnamo tarehe 27/11/2020 kabla ya muombaji hajateuliwa kuwa msimamizi wa mirathi hiyo.Wosia ya marehemu huyo upo mahakamani waweza kukaguliwa tarehe 19/11/2020.

Sahihi ya Hakimu
HAKIMU

116008702

*Uza,*
*Chenye Thamani Kubwa*
*Kwa Kutangaza Nasi Kwa*
*Bei Poa*
*Tupigie 0782253676*

Kwa Habari Motomoto
usikose Gazeti lako
la Nipashe kila siku
Tupigie
0782253676
Nipashe
MWANGA WA JAMII

TAHADHARI: Wasomaji wanatakiwa kuuliza na kuchukua ushauri sahihi kabla ya kutuma fedha, au kuingia katika gharama yoyote kati yake na mtangazaji THE GUARDIAN LIMITED hawatahusika kwa malipo au manunuzi yoyote kati ya muuzaji na mnunuaji kwa matangazo yaliyochapishwa katika gazeti hili.

# HADITHI

ILISEMWA hapo zamani kuwa dunia inaharibiwa na vitu viwili tu. Mapenzi na mali. Vitu hivi vinaweza kumfanya binadamu aende popote, afanye chochote kile ili awenavyo, wengine wanakwenda mbali zaidi mpaka ikiwezekana hata kutoa uhai wa wenzao.

Shani, binti wa kitajiri anapitia kwenye mikasa mikubwa mizito ya kupotezwa kwa wazazi wake na kumsababishia ukiwa na mawazo tele. Wakati ikionekana binti huyo pekee kwa wazazi wake akielekea kurithi utajiri wa wazazi wake, kiu ya damu inaanza kuwaingia baadhi ya ndugu za wazazi wake ili apoteze maisha, wao waweze kumiliki mali hizo. Hapo ndipo uhai wa Shani unapokuwa matatani na patashika nguo kuchanika inapoanza. Fuatilia mkasa huu kuburudisha, kuelimisha na kusikitisha.

## Mauaji Harusini-**39**

**Mtunzi anapatikana (0716 350534)**

**Na Adam Fungamwango**

ALIANZA kupunguza kasi ya gari ili bodaboda ikaribie. Alishajua nini walihitaji. Wakati ikifika karibu na dirisha, ghafla alifunga breki.

Waliokuwa kwenye bodaboda hawakutegemea hilo, hivyo alipitiliza. Hapo hapo milio kadhaa ya risasi ilimiminika.


Ilipopigwa ni eneo ambalo lilitakiwa gari la Eddy na mpenzi wake Shani liwe. Kitendo bila kuchelewa, Eddy alimbeba Shani kama simba ananyombeba nyati, alibimbirika naye kwenye viti vya nyuma. Alijua kabisa kuwa watu hao walidhamiria kuwateketeza kwa risasi. Hivyo alijua risasi zitakazofuata baada ya kuwakosa, zitamiminika eneo la mbele la gari lao. Na ndivyo ilivyokuwa. Wakati gari la lilikuwa likifuata nyuma likimimina risasi zake kupitia kioo cha nyuma na kwenda kuvunja kioo cha mbele. Bodaboda iliyokuwa imepitiliza mbele nayo iligeuka nyuma na kuifuata gari waliyokuwepo kina Eddy. Nao wakamimina risasi za kutosha na kuichakaza gari hiyo kwa tundu.

Lilikuwa ni eneo la Kinondoni Mwembe Jini. Wengine wakaita Kinondoni Makaburini. Hakukuwa na watu wengi sana eneo hilo kutokana na mazingira ya eneo hilo.

Waliokuwepo walianza kukimbizana kuokoa maisha yao, kwani kila mmoja alitambua kuwa zilikuwa ni risasi zinamiminwa.

Kama walivyotegemea Eddy ni kwamba akili ya wote wale itakuwa mbele kwenye kiti cha dereva na abiria wake. Ndiyo maana haraka alihamia kwenye viti vya nyuma. Wakati risasi zinamiminwa tayari yeye na Shani walikuwa huko. Chenga chenga za vioo ndizo zilizowaangukia. Haraka alifungua mlango wa nyuma kwa uangalifu. Akiwa amemshikilia Shani madhubuti, aliruka kutoka garini na kubimbirika haraka kikomandoo. Hakuonekana na binadamu yoyote. Baada ya kuona hakukuwa na majibu. Watu wawili waliokuwa wamepanda bodaboda walipaki na kulisogelea kwa uangalifu gari lililokuwa limetobolewa na risasi nyingi. Watu wanne walishuka kwenye gari lililokuwa likifuata nyuma. Hawakuonekana kuwa na wasiwasi sana. Ila walikuwa na tahadhari. Walilizunguka gari kuhakikisha kuwa hatoki mtu ndani, huku kila mmoja kiwa amekaa tayari kwa chochote kitakachotokea. Mmoja alikaa pembeni akiwa na bastola yake kubwa. Huyu alionekana kuwa ndiye mtaalam wa shabaha. Ndiye alionekana kulinda wenzake. Mtu mwingine alikuwa na bastola ndogo ya kawaida. "fungua mlango", mmoja aliamuru.

Aliyekuwa akiendesha bodaboda ndiye aliyefungua mlango wa dereva ili kuangalia mawindo yao waliyokuwa wameyafuata. Walijua kabisa kuwa kama ndani hawakuwakuta marehemu, basi watawakuta nyang'anyang'a, wakiwa hoi bin taabani kwa matundu ya risasi. Kama ni hivyo nia yao wawamalizie na kuwawahisha ahera wote wawili.




**Hilo ndilo alilokuwa akilisubiri. Mmoja wao alipita karibu na alipokuwa Eddy. Akiwa hajui hili wala lile, ghafla Eddy alijitokeza mbele yake. Nia kwanza ilikuwa ni kutia hofu. Mara nyingi hofu humfanya mtu kutokuwa au kuishiwa na nguvu.**

************************

Kutokana na giza lililoanza kutanda eneo hilo, hakuna yoyote aliyemuona Eddy aliyekuwa ameruka akiwa amemshikilia Shani kutoka nje ya gari muda mfupi tu baada ya kundi hilo kupfika.

Eddy alikuwa amenong'oneza Shani kutopiga kelele au kusema chochote kile, kwani akifanya vivyo tayari watakuwa wamehesabika kuwa ni marehemu.

Alitambaa kikomandoo kuelekea ndani kidogo ya makaburi. Ilibaki hatua chache tu kabla ya kufika kwenye eneo la makaburi ya Patiyo Kupila na mkewe Grace.

Ni eneo ambalo lilichaguliwa kuzikwa pamoja mtu na mkewe ambao waliuawa zaidi ya miezi sita iliyopita wakiwa ametoka kufunga ndoa kwenye kanisa la Mtakatifu Joseph jijini Dar es Salaam. Maharusu hao waliuawa maeneo ya Kibada, Kigamboni wakiwa mita chache tu kutoka ndani ya gari, kabla ya kufika kwenye eneo maalum waliloandaliwa kukaa.

Watu waliojulikana walifyatua risasi na kutoa uhai wao na kutoweka, mauaji ambao hadi leo yamekuwa kitendawili.

Eneo hilo la Makaburi ya Kinondoni ndipo walipozikwa pamoja, mume kushoto, mke kulia.

Hata mahusiano ya Eddy na Shani walianzia eneo hilo la makaburi. Shani alikuwa amefika hapo kwenye kaburi la baba yake mzazi Patiyo baada ya siku arobaini za mazishi. Eddy alifika hapo kumsailia shangazi yake Grace. Mtoto wa mwisho kwenye familia ya baba yake mzazi. Alipokuwa nchini Marekani alipata taarifa hizo za kuuawa akiwa ametoka kuolewa, hivyo aliporejea alizuru kaburi hilo na kukutana na mrembi huyo.

Mmoja alikuwa kushoto na mwingine kulia. Makaburi alikuwa yakuwa yanafanana na kuandikwa kabisa kuwa ni mtu na mkewe waliouawa. Lakini wao walikuwa hawafahamiani. Walipotaka kufahamiana, ndipo kila mmoja alipomhitaji mwenzake. Wakapendana mtu na binamu yake. Wakawa wapenzi.

Eddy alimkokota Shani mpaka kwenye makaburi ya maharusi. "Lala hapa katikati ya makaburi haya. Hakuna atakayekuona. Usiogope. Wala usipige kelele au kusema chochote. Hata kama unahisi kuna hatari. Acha mimi niende kupambana. Nitarudi." Alimnong'oneza.

Haraka, Eddy alirejea kule kwenye mapambano kwa kutumia tumbo kikomandoo. Wakati huo kikundi cha watu waliotaka roho za Eddy na mpenzi wake Shani kilikuwa kwenye msako ya kutaka kuona anglau maiti zao.

Mmoja aliyeamriwa kuingia ndani ya gari na kupekua, hakuambulia kitu.

"Ni kwamba hakuna mtu, kwa sababu kwa jinsi gari ilivyotandikwa risasi, hata kama maiti zao zisingeonekana kwa kubanwa kwenye vyuma na mabati, basi hata damu zingekuwa zimetapakaa." Alisema aliyeingia kupekua ndani ya gari hiyo."

"Kifupi ni kwamba hawamo kwenye gari." Alidakia mwingine.

Kuna hali fulani ya wasiwasi ilianza kuwaingia. Kitendo cha mawindo yao kupotea. Halafu eneo hilo lenye majani, vichaka na miti mingi pamoja na giza lililoanza kuingia iliwatisha.

Kikubwa zaidi ni kwamba waliona kabisa kuwa huenda hawachezi na mtu wa kawaida.

Awali ilionekana ni kazi nyepesi tu. Ni kwenda kummaliza msichana Shani. Ndani ya gari la Shani yumo mpenzi wake mmoja ambaye mara kwa mara ndiye anayemchukua na kumrejesha kazini. Ilitolewa amri kuwa kama naye akileta usumbufu, basi na yeye asafiri pamoja na mpenzi wake kuzimu.

Kumuua msichana kama yule ilionekana ni jambo dogo tu, japo ugumu ulikuwepo kwa sababu hakuwa peke yake. Lakini haikudhaniwa kuwa ingekuwa ngumu kiasi hicho.

Kutambaa kwa tumbo, kulimfikisha karibu na barabara. Karibu na eneo lile ambalo gari lake limeteketezwa na risasi. Ni mita chache tu kutoka kwa watu sita, wanne kutoka kwenye gari na wawili kutoka kwenye bodaboda wakihangaika kutafuta waliokuwa wakiwatafuta.

"Kuweni na tahadhari. Na sasa natoa amri, wote wawili wakionekana wauawe." Eddy aliisikia amri hiyo.

Mmoja wa watu waliokuwa na bunduki aliruka mfereji wa maji uliokuwa kando ya barabara hiyo na kuelekea kwenye mti mmoja uliokuwa kando. Akiwa na tahadhari, lakini akijiamini kupita kiasi aliufuata mti huo kwa makini.

Eddy hakuna na bunduki. Aliitaka kwa udi na uvumba. Kwa akili yake kikomandoo. Alichukua kijiwe na kukirusha upande wa kushoto huku yeye akiwa kulia.

Kishindo hafifu cha kijiwe hicho kilishtua jamaa mwenye bunduki. Akaangalia kushoto na kulia. Kwa akili yake alivyofundishwa ni kwamba jiwe likitupwa kushoto, basi mtupaji atakuwa yupo kulia.

Sivyo alivyofikiri. Eddy alishahama siku nyingi. Alivyorusha na yeye akaelekea upande huo huo kwa kutambaa.

Jamaa alipogeuka na kuelekea alipodhani ndipo kijiwe kilipotupwa, Eddy alimfuata taratibu akiwa anatambaa kama mamba anavyowinda.

Ghafla alisimama. Wakati jamaa akihisi kama kuna kitu nyuma, tayari alikuwa amepigwa karate ya kichwa ilivyomfanya kutokwa na fahamu papo hapo. Hakutaka aanguke kama mzigo ili kutowashtua wenzake. Alimkamata na kumpeleka chini taratibu, akamlaza chini ya mti.

Akaichukua bunduki iliyokuwa mikononi mwa adui. "Sasa kazi imekuwa rahisi kuliko urahisi wenyewe." Alijisemea.

Tayari alikuwa ameshapunguza mtu mmoja, walibaki watano badala ya sita.

"Tawanyikeni." Amri ilitoka kwa mkubwa wao.

Hilo ndilo alilokuwa akilisubiri. Mmoja wao alipita karibu na alipokuwa Eddy. Akiwa hajui hili wala lile, ghafla Eddy alijitokeza mbele yake. Nia kwanza ilikuwa ni kutia hofu. Mara nyingi hofu humfanya mtu kutokuwa au kuishiwa na nguvu.

Kabla ya kupiga kelele, lilifuata teke la mdomo ili ahindwe kusema chochote au kupiga kelele kuwasiliana na wenzake. Sekunde chache baadaye teke hilo hilo lilitua kwenye mbavu na kuanguka chini kama mzigo.

Wakati wote huo, Eddy alijua watu hao hawakufa, ila watazinduka baada ya nusu saa au dakika arobaini na tano. Sasa walibaki wanne.

**ITAENDELEA JUMAMOSI**

# PULISIC AMUUMIZA KICHWA LAMPARD




**LONDON,** England

FRANK Lampard amesisitiza Christian Pulisic anaweza kuwa na mchango mkubwa sana Chelsea mara tu winga huyo atakapopona matatizo yake ya misuli yanayomsumbua.

Nyota huyo wa kimataifa wa Marekani amekosa mwanzo wa msimu huu, lakini alikuwa na uwezekano wa kurudi dimbani kuichezea Chelsea lakini akaumia tena Oktoba 31, mwaka huu kabla ya mchezo dhidi ya Burnley.

Matatizo ya misuli kwa Pulisic yalimwanza tangu Agosti, mwaka huu wakati wa mchezo wa fainali ya Kombe la FA dhidi ya Arsenal, baada ya kufunga bao la ufunguzi kwenye mchezo huo, na yameendelea kumsumbua.

Nyota huyo aliyesajiliwa kwa pauni milioni 58 kutoka Borussia Dortmund hatakuwapo kwenye mchezo wa leo Jumamosi dhidi ya Newcastle United na Lampard amesema anaweza kuwapo kwenye mchezo ujao.

Bila shaka majeruhi hayo yanaichanganya Chelsea, huku timu ya madaktari wakifanya kazi kubwa kumsaidia Pulisic kurudi katika uimara wake.

"Kwa Christian, tunaendelea kutafuta namna ya kumaliza tatizo," alisema Lampard.

"Kwa sasa yupo kwenye matatizo ya majeruhi ya mara kwa mara, lakini siku tutakapopata ufumbuzi wa tatizo lake, atakuwa msaada mkubwa zaidi kwetu."

# Baba asisitiza Haaland haondoki Dortmund

**DORTMUND,** Ujerumani

ERLING Haaland anataka kushinda mataji akiwa na Borussia Dortmund na hafikirii kuhusu kuondoka klabuni hapo, kwa mujibu wa baba yake mzazi, Alf-Inge Haaland.

Dortmund ilishinda mbio za kumsajili Erling Haaland kutoka Salzburg Januari iliyopita na amekuwa na mwanzo mzuri pale katika dimba la Signal Iduna Park, akifunga mabao 27 katika mechi 29 kwenye mashindano yote kwa klabu hiyo.

Raia huyo wa Norway amekuwa akihusishwa sana na kuwaniwa na klabu nyingi kubwa Ulaya.

Na sasa baba mzazi wa nyota huyo mwenye umri wa miaka 20, Alf-Inge Haaland, amesisitiza hakuna mjadala wa kuondoka kwa sasa.

"Wakati unapocheza vizuri, ni jambo la kawaida kwa klabu kubwa kukugongea mlango, lakini hatuzungumzii kuhusu uvumi wa usajili hapa," alisema akiiambia SPORT1.

"Kwa wakati huu, Erling hana mpango wowote wa kuangalia uwezekano wa kwenda katika klabu nyingine.

"Tumesaini mkataba wa muda mrefu na Dortmund na wana timu nzuri inayovutia kwa Erling kwa sasa. Hatutaki kuangalia upande mwingine kwa sasa."






# Tebas: LaLiga itasonga bila Lionel Messi

**MADRID,** Hispania

RAIS wa Ligi Kuu Hispania, LaLiga, Javier Tebas, amesema yuko tayari kuona ligi hiyo ikiendelea bila uwepo wa nyota wa Barcelona, Lionel Messi.

Tebas anayasema hayo ikiwa ni miezi kadhaa imepita tangu Messi kuwasilisha maombi ya kutaka kuondoka klabuni hapo kutokana na kile kilichotajwa kuwa hawaelewani na Rais wa Barcelona, Josep Maria Bartomeu ambaye alijiuzulu Oktoba, mwaka huu.

Tebas anahitaji Messi kubaki nchini Hispania na acheze kwenye LaLiga, lakini anasema hata akiondoka watazoea kuitazama ligi hiyo bila uwepo wake.

"Tungependelea kumwona Messi anabakia LaLiga, lakini aliondoka Cristiano Ronaldo na Neymar Jr hatukuona tofauti yoyote na tupo tayari kwa hilo," alisema akinukuliwa na Marca.

Nyota huyo wa kimataifa wa Argentina mwenye umri wa miaka 33 atakuwa huru mwishoni mwa msimu huu, huku Manchester City na Paris Saint Germain zikitajwa kuwinda saini ya fowadi huyo.

HABARI MICHEZO

# PSG yawania kumsajili Ramos

**PARIS,** Ufaransa

MLINZI wa Real Madrid, Sergio Ramos, amewekwa kwenye rada za mabosi wa PSG inayoshiriki Ligi Kuu Ufaransa maarufu Ligue 1, kwenye usajili wa dirisha la Januari, mwakani.

PSG inaamini kuwa ikipata saini ya nyota huyo itazidi kuwa imara ndani ya uwanja na kupata matokeo chanya kwenye mashindano ambayo watashiriki.

Kwa mujibu wa ESPN, mabosi wa PSG wameweka mezani kitita cha pauni milioni 18 ili kumpata Ramos, raia wa Hispania ambaye ana umri wa miaka 34.

Imeripotiwa kwamba, PSG wapo tayari kumpa mkataba wa miaka minne tofauti na mabosi wake wa sasa Madrid ambao wao dili lao wanalotaka kumpa ni la mwaka mmoja.

Mkataba wa Ramos unakamilika mwisho mwa msimu huu hivyo ikiwa hataongezewa mkataba mwingine itakuwa dili jepesi kwake kuibukia ndani ya PSG licha ya kwamba Kocha Mkuu wa Madrid, Zinedine Zidane anahitaji huduma ya beki huyo.






# LOW ATAKIWA KUJIUZULU KUIFUNDISHA UJERUMANI

**MUNICH,** Ujerumani

LICHA ya Shirikisho la Soka la Ujerumani (DFB), kusema halitamtimua Kocha Mkuu wa Timu ya Taifa, Joachim Low, mashabiki na baadhi ya nyota wa zamani wa timu hiyo wanataka ajiuzulu.

Hilo linakuja ikiwa ni siku nne tangu kikosi cha Ujerumani kupigwa kipigo cha mabao 6-0 na Hispania kwenye mchezo wa Ligi ya Mataifa Ulaya, Jumanne mjini Sevilla.

Mashabiki wamepanga kumwonyesha kadi nyekundu kocha huyo ikiwa ni ishara ya kutomtaka sambamba na baadhi ya wachezaji wa zamani wa timu hiyo wakidai ameiaibisha timu yao. Mashabiki wamechukia kwa sababu ni kipigo kizito zaidi katika historia ya timu hiyo, kwani mara ya mwisho kufungwa idadi hiyo ya mabao ilikuwa mwaka 1931 katika mchezo wa kirafiki dhidi ya Austria.

Loew alifanya kikao na Rais wa DFB, Fritz Keller, Jumatano mjini Munich huku kukiwa kumesalia muda wa miaka miwili kwenye mkataba wake wa sasa na huenda akaendelea kuwa na kikosi hicho kwenye mashindano ya Kombe la Euro mwakani.

Hata hivyo, kwa mujibu wa utafiti uliofanywa na Shirika la SID ambalo ni tawi la Shirika la Habari la AFP, asilimia 84.0 ya mashabiki nchini Ujerumani wanataka kocha huyo kufutwa kazi na Mkurugenzi wa Michezo, Oliver Bierhoff pia kuachia madaraka.

Wakati asilimia 13.3 pekee wanataka kocha na Mkurugenzi wa Michezo waendelee kubakia pamoja kwani walishashinda Kombe la Dunia mwaka 2014 nchini Brazil.

Hata hivyo, huenda taarifa hizi zikawa chungu kwa Liverpool na Bayern Munich ambao huenda mmoja wapo akashuhudia kocha wake akienda kuchukua mikoba ya Loew endapo mamlaka nchini Ujerumani zitaamua kuachana naye.

# Fifa kumlipa mshahara Gomez

**NYON,** Uswisi

SHIRIKISHO la Soka la Kimataifa (Fifa), linataka kuilipa Klabu ya Liverpool ambao ni mabingwa watetezi wa Ligi Kuu England kiasi cha pauni milioni mbili.

Fedha hizo ni kwa ajili ya malipo ya mshahara wa beki wao, Joe Gomez, ambaye aliumia kwenye Timu ya Taifa ya England ilipokuwa kwenye mazoezi na anaweza kukaa nje kwa muda mrefu.

Beki huyo ambaye aliumia goti analipwa mshahara wa pauni 80,000 kwa wiki akiwa ni miongoni mwa wachezaji wanaolipwa mkwanja mrefu ndani ya timu hiyo.

Fedha hizo zitalipwa na Fifa kwa kuwa wachezaji wa kikosi cha England wapo kwenye mradi wa msaada wa shirikisho hilo la soka duniani, lakini wakiwa na bima ambazo zinasimamiwa na Fifa.



# DONDOO ZA SOKA MAGAZETI YA ULAYA



# GUARDIOLA, CITY MAMBO MAZURI

●●● Ni baada ya kusaini mkataba mpya wa kuendelea kuiongoza klabu hiyo na kuzima tetesi za...

**MANCHESTER,** England

KOCHA Mkuu wa Manchester City, Pep Guardiola, amefuta tetesi zilizokuwa zikimhusisha za kurudi kwa miamba ya soka la Hispania, Barcelona kwa kusaini mkataba mpya, klabu hiyo ya Ligi Kuu England imethibitisha.

Mkataba wa sasa Guardiola ulikuwa unamalizika mwishoni mwa msimu huu, lakini City imetangaza juzi kwamba kocha huyo amekubali kuendelea kubakia hapo kwenye dimba la Etihad kwa miaka mingine miwili.

**Na sasa mkataba wake huo utamfanya kuendelea kuwa kwenye viunga vya City hadi mwaka 2023.**

Tangu alipochukua mikoba ya kumrithi Pellegrini mwaka 2016, kocha huyo kutoka Katalunya ameiongoza klabu hiyo kushinda taji la Ligi Kuu England mara mbili na mara ya mwisho ilikuwa msimu wa 2018-19.

"Kuongeza mkataba kwa Pep ni jambo la kawaida katika safari ya soka ambayo amehusika nayo kwa miaka mingi," alisema Mwenyekiti wa City, Khaldoon Mubarak. "Ni zao la maelewano na kuaminiana na heshima kudumu kati yake na klabu nzima."

Guardiola mwenye umri wa miaka 49, tayari ameshashinda taji la EPL mara mbili, Kombe la FA na taji la Kombe la Ligi tangu alipojiunga na City mwaka 2016.

Kocha huyo wa zamani wa Barcelona na Bayern Munich, sasa inakuwa mara ya kwanza kwa kwake kukaa kwenye timu moja kwa kipindi kirefu cha miaka nane tangu ambapo alianza kufundisha soka mwaka 2008.

Kwa ujumla, City wameshinda mechi 181 katika mechi 245 chini ya Guardiola na wana wastani wa kushinda mechi kwa asilimia 73.87.

## ZISIKUPITE

### CITY YAMGANDA MESSI

KLABU ya Manchester City wameazimia kumsajili mshambuliaji wa Barcelona na Timu ya Taifa ya Argentina, Lionel Messi, mwenye umri wa miaka 33, baada ya kocha Pep Guardiola kukubali mkataba mpya. ***(Mirror)***

### CAMAVINGA AGOMBEWA

MANCHESTER United watapambana na Paris St-Germain na Real Madrid katika kuwania saini ya kiungo wa kati wa Ufaransa kutoka Klabu ya Rennes, Eduardo Camavinga, 18. ***(Marca, via Mail)***

### RAMOS ANUKIA EPL

KLABU kadhaa za Ligi Kuu England zinawania kutaka kumsajili mlinzi wa Hispania, Sergio Ramos, iwapo nyota huyo wa Real Madrid mwenye umri wa miaka 34 hataongeza mkataba wake kule Santiago Barnabeu. ***(90min)***

### ALABA NYOTA IMENG'AA

REAL Madrid watamnunua beki wa Bayern Munich na Austria, David Alaba mwenye umri wa miaka 28, kama Sergio Ramos ataondoka. ***(Marca)***

### EVERTON YAMWANIA JAMES

EVERTON wanaangalia uwezekano wa kumsajili winga wa Manchester United na Timu ya Taifa ya Wales, Daniel James mwenye umri wa miaka 23, wakati wa dirisha la Januari. ***(Football Insider)***

### GIROUD KUONDOKA CHELSEA

MSHAMBULIAJI Olivier Giroud mwenye umri wa miaka 34, yuko tayari kuangalia uwezekano wa ofa ya kuondoka Chelsea Januari kwa lengo la kupata nafasi ya kucheza zaidi katika kikosi cha Ufaransa kwa ajili ya msimu ujao wa Kombe la Ulaya. ***(Guardian)***

### ALMIRON NJIA MOJA

NEWCASTLE United ipo tayari kusikiliza ofa kwa ajili ya kiungo wa kati wa Paraguay, Miguel Almiron mwenye umri wa miaka 26, ambaye tayari amepewa ofa na klabu kadhaa. ***(90min)***

### KHEDIRA AITAMANI EPL

KIUNGO wa kati wa Juventus Mjerumani Sami Khedira ambaye ana umri wa miaka 33, anataka kuhamia katika Ligi Kuu England na anaweza kuwa chaguo la Everton au Manchester United. ***(Sun)***

### MNIGERIA KUINUNUA ARSENAL

BILIONEA wa Nigeria, Orji Kalu, anataka kununua asilimia 35 ya hisa za Arsenal na "kurejesha vikombe" katika klabu hiyo. ***(Mirror)***

### LUIZ, CEBALLOS KIMENUKA

MLINZI wa Arsenal, Mbrazil David Luiz (33), alihusika katika malumbano na Dani Ceballos, 24, walipokuwa katika uwanja wa mazoezi na akamgonga kwenye pua kiungo huyo wa kati raia wa Hispania. ***(The Athletic - subscription required)***

### MILAN YAMTAKA SUPRIAHA

AC Milan wanamtaka mshambuliaji wa timu ya vijana walio chini ya umri wa miaka 20 wa Dynamo Kyiev na Timu ya Taifa ya Ukraine, Vladyslav Supriaha. ***(Calciomercato)***

HABARI MICHEZO

## Polisi Zanzibar yaipania Mafunzo

**Na Hawa Abdallah,** ZANZIBAR

KOCHA Mkuu wa Polisi 'Wajela Jela', Yusuph Sape, amesema timu yake imejipanga imara kuhakikisha inapata ushindi dhidi ya Mafunzo katika mechi ya Ligi Kuu Zanzibar itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Amaan Visiwani hapa.

Sape alisema amewaandaa vizuri wachezaji wake kwa sababu anahitaji kuona wanaanza vyema katika msimu huu wa ligi wa mwaka 2020/21.

Kocha huyo alisema kikosi chake kipo tayari kupambana katika mechi hiyo na zitakazofuata kwa sababu malengo yao ni kutwaa taji la Ligi Kuu Zanzibar msimu huu. Alisema mpaka sasa katika kikosi chake cha kwanza hakuna mchezaji atakayekosa mchezo huo hivyo anaamini ataibuka na ushindi kwenye michezo ya mwanzo wa ligi.

"Wachezaji wangu wote wapo fiti hakuna majeruhi, inamaana kikosi changu cha kwanza kitashuka kama nilivyokipanga, na hii inanipa matumaini makubwa ya kupata alama tatu japokuwa mpira ni mchezo wa makosa ambao mpinzani wako anaweza kutumia makosa yako na kuubadilisha mchezo," alisema.

Hata hivyo alisema anawaheshimu wapinzani wake kutokana na uzoefu waliokuwa nao kwenye ligi na vile vile wana wachezaji waziri ambao wanauwezo wa kubadilisha matokeo wakati wowote.

Mechi nyingine ya ligi hiyo itakayochezwa leo ni kati ya Chuoni dhidi ya Malindi wakati kesho Mlandege itawakaribisha Hard Rock huku Zimamoto ikiwavaa KMKKM.

## Hitimana anogewa kufundisha Bongo

**Na Adam Fungamwango**

ALIYEKUWA Kocha Mkuu wa Namungo FC, Mnyarwanda, Hitimana Thiery, amesema anapenda kuendelea kufanya kazi hapa nchini kutokana kuwa na Ligi Kuu bora na yenye kushirikisha timu zenye ushindani.

Hitimana ambaye aliachana rasmi na Namungo hapo juzi, alisema tayari ameanza mazungumzo na baadhi ya timu zilizoko kwao Rwanda, lakini anatoa kipaumbele kwa timu za Tanzania.

"Nakwenda nyumbani Rwanda kwa ajili ya mapumziko, nasikia pia kuna timu inanihitaji huko kwetu, nitakwenda kuisikiliza, lakini mimi ningependa sana kufundisha Tanzania kwa sababu kuna ligi bora, pamoja na timu zenye ushindani sana, hii inatujenga hata sisi makocha kila siku tunaumiza vichwa na kujifunza vitu vipya," alisema Hitimana.

Taarifa zilizopatikana jijini zinasema Hitimana anawindwa na klabu ya Mbeya City ambayo hivi karibuni pia ilitangaza kuachana na kocha wake mkuu, Amri Said.

Kwa sasa Mbeya City iko chini ya Kocha Msaidizi, Mathias Wandiba na imeelezwa mmoja wa makocha waliopendekezwa kutua klabuni hapo ni Hitimana.

Hitimana aliiongoza vyema Namungo katika msimu uliopita na ameipatia tiketi ya kushiriki mashindano ya kimataifa ya Kombe la Shirikisho Afrika.

# KATWILA AITABIRIA MAKUBWA IHEFU FC

**Na Adam Fungamwango**

WAKATI leo watakuwa ugenini kuwavaa Polisi Tanzania, Kocha Mkuu wa Ihefu FC, Zuberi Katwila, amesema hatakuwa tayari kuiona timu hiyo inayoshiriki Ligi Kuu Tanzania Bara inashuka daraja na kuahidi kutumia ujuzi wake wote ili kusalia kwenye ligi hiyo.

**Kocha huyo wa zamani wa Mtibwa Sugar, alisema kipindi cha mapumziko ya kupisha kalenda ya kimataifa, alikitumia kurekebisha makosa aliyoyabaini kwenye kikosi chake baada ya kutua katika timu hiyo ya jijini Mbeya.**

"Katika mapumziko haya nimekaa na vijana na kurekebisha vitu kadhaa na natumaini kwenye mechi zinazokuja tutapata matokeo mazuri," alisema Katwila, mchezaji wa zamani wa Mtibwa Sugar ya Manungu mkoani Morogoro.

Alisema kila mechi wanayocheza ni ngumu na hivyo amewandaa wachezaji wake kukabiliana na ushindani huo ili mwisho wa msimu wawe kwenye nafasi nzuri.

Hata hivyo, Katwila alitua Ihefu akitokea Mtibwa Sugar ambayo pia haikuwa na mwanzo mzuri wa ligi msimu huu.

Ihefu ndiyo timu inayoburuza mkia kwenye msimamo wa Ligi Kuu ikiwa na pointi tano tu, kati ya mechi 10 walizocheza baada ya kushinda mechi moja, sare mbili na kufungwa michezo



saba.

Ihefu ilionja ushindi wa kwanza kwenye ligi hiyo Septemba 13, mwaka huu kwa kuwafunga Ruvu Shooting ya Pwani bao 1-0.

Baada ya hapo timu hiyo ilicheza mechi sita bila kupata ushindi, ikifungwa mechi zote na kutoka sare moja tu, dhidi ya Mbeya City.

Mechi nyingine za Ligi Kuu Tanzania Bara zitakazochezwa leo ni kati ya Coastal Union dhidi ya Simba ambayo itafanyika kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini Arusha huku JKT Tanzania wakiwa nyumbani kwenye Uwanja wa Jamhuri, Dodoma watawaalika Gwambina wakati vinara wa ligi hiyo, Azam FC, watawafuata KMC kwenye Uwanja wa Uhuru.




Msanii maarufu wa vichekesho nchini, Joti, akizungumza kuhusiana na idadi ya zawadi ya simu janja 240 zilizotolewa na nyingine 960 zimebaki katika kampeni ya Jaza Tukujaze Tena inayoendeshwa na Kampuni ya simu za mkononi ya Tigo. Kushoto ni balozi wa kampeni hiyo, Meena Ally na Meneja Huduma kwa Wateja wa Kanda ya Pwani, Beatrice Kinabo. **PICHA: MPIGAPICHA WETU**

# SportPesa sasa kwa WhatsApp

**Na Mwandishi Wetu**

KATIKA kuhakikisha inakuwa karibu zaidi na wateja, Kampuni ya Michezo na Burudani ya SportPesa Tanzania, imezidi kutanua wigo wake wa mawasiliano kwa kujisogeza karibu yao zaidi baada ya jana kuzindua rasmi namba ya WhatsApp kwa ajili ya kuwasiliana nao.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Meneja Uhusiano wa SportPesa, Sabrina Msuya, alisema hatua hiyo ni ya kihistoria kama kampuni katika kuendelea kuwa karibu zaidi na wateja wake, lengo likiwa ni kuhakikisha wanaboresha nyanja zote za mawasiliano.

"Leo (jana), itakuwa mara ya kwanza kabisa kuzindua namba mpya itakayotumiwa na wateja wetu wapya na wale wa zamani kwa huduma ya WhatsApp. Namba yetu ni ***0745 042 855*** na itakuwa wazi kuanzia sasa kwa wateja wetu wa mitandao yote ya simu.

"Kupitia namba hii wateja wetu wanaweza kutuma picha ili kutatua matatizo yao kama moja ya huduma ya SportPesa," alisema Msuya.

Alisema huduma hiyo inaweza kumrahisishia mteja katika kueleza tatizo lake na pia kulitatua kwa haraka zaidi.

"Kama ilivyo ada, huduma zetu ni kwa saa 24 kwa wiki, ili kumfikia mteja wetu kila wakati anapohitaji huduma. Ubunifu ndio sifa kuu na mteja siku zote ni mfalme kwetu."

Mbali na huduma mpya ya WhatsApp, alisema SportPesa pia ina namba nyingine kwa ajili ya mawasiliano ya sauti yaani kupiga na kupokea simu ambazo ni ***0764 115588***, ***0677 115588*** na ***0685 115588***.

# Michezo

Jumamosi Novemba 21, 2020

Nipashe


## Guardiola, City mambo mazuri




# Yanga yaendelea kumwota Morrison

**Na Saada Akida**

WAKATI uongozi wa Yanga ukimtangaza, Haji Mfikirwa kuwa Kaimu Katibu Mkuu wao, klabu hiyo imelitaka Shirikisho la Soka Tanzania (TFF), kusikiliza shauri na malalamiko yao kuhusiana na mkataba wa winga mshambuliaji wa Simba, Bernard Morrison.

Mfikirwa amechukua mikoba ya Simon Patrick ambaye amesimamishwa na mabosi wa klabu hiyo ili kupisha uchunguzi wa tuhuma zinazomkabili.

Akizungumza jijini Dar es Salaam jana, Makamu Mwenyekiti wa Yanga, Frederick Mwakalebela, alisema wanaiomba TFF kukutana na kujadili kesi ambazo ziliwasilishwa na klabu yao kabla ya dirisha dogo la usajili halijafunguliwa ifikapo Desemba 15, mwaka huu.

Mwakalebela aliitaja kesi nyingine ambayo wanahitaji itolewe uamuzi ni kuhusiana na tuhuma zilizowekwa wazi na golikipa wao, Ramadhani Kabwili, ambaye klabu mojawapo ilitaka kumlaghai.

"Tuna wasiwasi dirisha la usajili likifunguliwa watatumia nafasi hiyo kupeleka mkataba uliokamilika katika mtandao," alisema Mwakalebela.

Aliongeza Yanga inajipanga kukabiliana na hujuma mbalimbali wanazofanyiwa ili wafikie malengo yao ya kutwaa ubingwa wa Ligi Kuu Tanzania Bara msimu huu.

Naye Mshauri wa Yanga, Senzo Mbatha alisema kikosi cha Yanga kiko vizuri lakini kuelekea mchezo wao wa kesho dhidi na Namungo FC, watamkosa kiungo wao wa kimataifa kutoka Rwanda, Haruna Niyonzima.

"Nimezungumza na Kocha, Cedric Kaze, amehakikisha kikosi kipo vizuri, Niyonzima hatakuwapo, alienda Rwanda na alipata ajali, lakini hakupata majeraha yoyote na anaendelea vizuri," alisema Senzo.

Kuhusu suala la mchakato wa mabadiliko, alisema unaendelea vizuri na kati ya Jumatatu na Jumanne wanatarajia wawakilishi wao wawili kwenda Hispania kuchukua ripoti ya mfumo huo ilipofikia.

Aliongeza tayari klabu hiyo imetangaza zabuni kwa ajili ya ujenzi wa hosteli na uwanja wa mazoezi utakaojengwa katika eneo la Kigamboni jijini, Dar es Salaam.



Kiungo wa Real Madrid, Luca Modric (kulia), akijaribu kumiliki mpira kwenye mazoezi ya timu hiyo iliyokuwa inajiandaa na mechi ya Ligi Kuu Hispania maarufu Laliga dhidi ya Villareal itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Estadio de la Ceramica. **PICHA: MTANDAO**

# SIMBA, AZAM VITANI LIGI KUU

## Kila timu yatamba kusaka ushindi ili kujiimarisha kwenye msimamo wa...

**Na Somoe Ng'itu**

SAFARI ya kuwania pointi tatu muhimu inatarajia kuendelea kwa mabingwa watetezi, Simba kukabiliana na Coastal Union ya Tanga katika mechi ya Ligi Kuu Tanzania Bara itakayochezwa leo kwenye Uwanja wa Sheikh Amri Abeid jijini, Arusha.

Coastal Union imelazimika kuhamia Arusha baada ya Uwanja wake wa CCM Mkwakwani kufungwa kutokana na kutokidhi sifa zilizowekwa na Bodi ya Ligi Kuu Tanzania.

Kocha Mkuu wa Simba, Sven Vandenbroeck, aliliambia gazeti hili kikosi chake kilifika salama jijini Arusha na kiko tayari kwa mchezo wa leo.

Sven alisema amejiandaa vyema kukutana na ushindani katika mchezo huo kwa sababu kwao, mabingwa watetezi, michezo yote ni migumu.

Kocha huyo alisema anahitaji kupata ushindi katika mechi ya leo ili kujiimarisha kwenye mbio za kutetea taji hilo wanalolishikilia kwa misimu mitatu mfululizo.

"Tunatarajia kukutana na ushindani, mechi haitakuwa nyepesi, kila timu imejipanga kufanya vizuri na zaidi inapokutana na sisi, tutaingia kwa tahadhari na tuko tayari kwa mapambano," alisema kocha huyo raia wa Ubelgiji.

**Juma Mgunda, Kocha Mkuu wa Coastal Union, alisema kikosi chake kimejiandaa kuwashangaza mabingwa hao watetezi kwa kuchukua pointi zote katika mechi hiyo.**

Mgunda alisema kama wachezaji wake watatulia na kuongeza umakini, anaamini ataifunga Simba na kujiweka kwenye nafasi nzuri katika msimamo wa ligi hiyo inayotoa mwakilishi wa Tanzania Bara katika mashindano ya kimataifa.

"Tuko tayari kwa mchezo, ni mchezo ambao unahusisha wachezaji wanaojuana, kikubwa ni kuongeza umakini, mpira unapokosea unampa nafasi mpinzani wako kukuadhibu, hatutaki hilo litokee katika mechi hii," Mgunda alisema.

Naye Kocha Msaidizi wa Azam FC, Vivier Bahati, alisema wamejiandaa vizuri kuekelea mchezo wao dhidi ya KMC utakaochezwa leo kwenye Uwanja wa Uhuru jijini.

Aliwataja wachezaji watakaokosekana katika mechi hiyo ambao ni majeruhi ni pamoja na kiungo, Salum Aboubakar 'Sure Boy', beki, Oscar Masai na Frank Domayo ambaye aliumia kwenye mazoezi ya jana.

Aliongeza wanatarajia kukutana na ushindani katika mchezo huo kutokana na rekodi nzuri ya KMC inapokuwa kwenye uwanja wake wa nyumbani.

Kaimu Kocha Mkuu wa KMC, John Simkoko ametamba timu yake itaibuka na ushindi katika mechi hiyo.

"Katika mchezo wa kesho (leo), hakuna cha pira Ice cream, strawbery wala pira mkate, KMC itakwenda kuonyesha pira spana, tunawaomba mashabiki wajitokeze kwa wingi kuisapoti timu yao, kikosi chetu ni kizuri hivyo Azam wajipange, wasije kutoa sababu pindi watakapofungwa," Simkoko alisema.

Mechi nyingine za ligi hiyo zitakazochezwa leo ni kati ya Polisi Tanzania dhidi ya Ihefu FC wakati JKT Tanzania watawakaribisha Gwambina kwenye Uwanja wa Jamhuri jijini, Dodoma.


GAZETI HILI HUTOLEWA NA KUCHAPISHWA NA THE GUARDIAN LIMITED, S.L.P 31042

770856 541002 >